SURA YA KWANZA

SHERIA YA UTAFSIRI WA SHERIA

[SHERIA KUU]

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina la sheria na tarehe ya kuanza kutumika kwa Sheria
2. Matumizi
3. Jamhuri kufungwa na Sheria

SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA JUMLA YA TAFSIRI

4. Ufafanuzi utumikao katika sheria.
5. Matumizi.
6. Sheria hunena daima
7. Sehemu ya matamshi na miundo ya fasihi.
8. Jinsia na tarakimu.
9. Rejeo ya neno Waziri katika sheria.
10. Marejeo kwa tarakimu, kujumuishwa.
11. Tafsiri ya rejeo ndani ya kifungu, n.k.
12. Rejeo kwenye sheria kama ilivyorekebishwa.
13. Tafsiri ya neno “au”.

SEHEMU YA TATU
KUANZA KUTUMIKA NA KUTAJWA KWA SHERIA

14. Tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria.
15. Muda wa kuanza kutumika kwa sheria.
16. Kuanza kutumika kwa sheria palipo na kifungu cha masharti ya kutolewa kwa taarifa ya kuanza kutumika.
17. Tafsiri ya uwezo wa kupanga tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria.
18. Ushahidi wa tarehe ya kusainiwa.
19. Utekelezaji wa uwezo kabla ya kuanza kutumika.
20. Kutajwa kwa sheria.
21. Marejeo ya sheria kwa siku ya kuanza kutumika.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA UTUNGAJI NA UTUMIKAJI WA SHERIA.

22. Sheria kuwa sheria za umma.
23. Vifungu kujitosheleza kama sheria kamili.
24. Sheria yaweza kurekebishwa au kufutwa katika kikao hicho hicho.
25. Utangulizi na Majedwali.
26. Vichwa, maelezo ya pembeni, rejeo chini ya ukurasa na marekebisho ya makosa.

SEHEMU YA TANO
MAREKEBISHO NA KUFUTWA KWA SHERIA

27. Fasiri ya sheria inayorekebisha sheria nyingine pamoja na marekebisho yake.
28. Kufutwa kwa sheria kama ilivyorekebishwa.
29. Kufuta kwa kufuta.
30. Kufuta na kubadilisha.
31. Athari ya masharti mbadala.
32. Vifungu vya jumla vinavyobakizwa baada ya kufutwa.
33. Athari ya kufutwa kwa sheria kwenye sheria ndogo.
34. Athari ya kumalizika kwa muda wa kutumika kwa sheria.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YANAYOHUSU SHERIA NDOGO

35. Rais anaweza kutunga sheria ndogo.
36. Masharti ya jumla kuhusu uwezo wa kutunga sheria ndogo.
37. Utangazaji na kuanza kutumika kwa sheria ndogo.
38. Kuwasilisha wa Kanuni Bungeni na kukataliwa.
39. Tafsiri ya sheria ndogo.
40. Kutajwa kwa sheria ndogo.
41. Marejeo ya sheria kujumuisha sheria ndogo.
42. Matendo chini ya sheria ndogo kuchukuliwa kama yamefanyika chini ya sheria.
43. Ada na tozo.

SEHEMU YA SABA
UWEZO NA WAJIBU WA KISHERIA

44. Muda wa utekelezaji wa uwezo au wajibu kwa mujibu wa sheria.
45. Rejeo kwa mshika ofisi itajumuisha warithi.
46. Tafsiri ya maneno ya kuwezesha.
47. Uwezo wa kutoa leseni, n.k.., ni wa hiari.
48. Uwezo wa kuteua unajumuisha uwezo wa kusimamisha au kufukuza n.k.
49. Uteuzi kwa jina au ofisi n.k., na uteuzi wa Mwenyekiti, n.k. Bodi, n.k...,.

50. Uwezo wa walio wengi, akidi, n.k.
51. Utekelezaji wa uwezo unaweza kusahihishwa.
52. Athari ya uteuzi wakati afisa anayestaafu akiwa likizo.
53. “Inaweza/Anaweza”, itakuwa na maana ya hiari, “ata/ita”, itakuwa na maana ya lazima.
54. Uwezo wa Bodi, n.k. hautaathirika kwa nafasi iliyowazi au mapungufu mengine.
55. Utekelezaji wa mamlaka fulani kwa anayekaimu.
56. Rejeo kwa eneo kwa kutumia mipaka.
57. Tafsiri ya uwezo wa kukasimu.
58. Ni nani ataweka lakiri ya kampuni.
59. Haki za Serikali.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI KUHUSU MUDA NA UMBALI

60. Kukokotoa muda..
61. Kuhesabu miezi.
62. Masharti pale muda haujapangwa.
63. Tafsiri ya uwezo wa kuongeza muda.
64. Kwenda kinyume na fomu.
65. Vipimo vya umbali.

SEHEMU YA TISA
TARATIBU NA ADHABU

66. Mashauri ya wadhifa wa kiofisi hayakomi baada ya kifo.
67. Kanuni za Mahakama.
68. Kutolewa kwa adhabu, si kizuizi cha kesi ya madai.
69. Upatikanaji wa faini na adhabu.
70. Kutia hatiani maradufu.
71. Matumizi ya sheria za adhabu kwa makampuni.
72. Masharti ya makosa chini ya sheria mbili au zaidi.
73. Marekebisho ya adhabu.
74. Maagizo ya adhabu ya juu, ya chini, ya siku, na za pamoja.
75. Vifungu vinavyohusu kujaribu.
76. Utoaji wa mali au vitu vilivyotwaliwa.
77. Uwajibikaji wa mwajiri au mkuu.
78. Ushahidi wa agizo, kibali au ridhaa ya mtumishi wa umma.
79. Utekelezaji wa mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka wakati hayupo.
80. Tamko la adhabu mwishoni mwa kifungu.
81. Makosa yanayoendelea.

SEHEMU YA KUMI
MASHARTI MBALIMBALI

82. Uwasilishaji wa nyaraka kwa njia ya posta.
83. Uwasilishaji wa nyaraka kwa ujumla.
84. Lugha ya sheria za Tanzania.
85. [Kufutwa kwa Sheria Na. 30 ya mwaka 1972.]

JEDWALI
(Kifungu cha 4)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

SURA YA KWANZA

_____

SHERIA YA UTAFSIRI WA SHERIA

Sheria ya majumuisho ya kanuni za msingi zinazohusu maana,ufafanuzi na matumizi ya sheria zilizotungwa, na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

[.....]

Sheria Na.
4 ya1996 na
17 ya 1996

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina la sheria na tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria

1.-(1) sheria hii inaitwa Sheria ya Utafsiri wa Sheria.

(2) Sheria hii itaanza kutumika tarehe ambapo Toleo la 2002 la Sheria zilizofanyiwa marekebisho zitakapoanza kutumika.

(3) Katika kifungu hiki "Toleo la 2002 la Sheria zilizofanyiwa marekebisho" ina maana ya Sheria za Tanzania zilizofanyiwa marekebisho na kuchapishwa.

Matumizi

2.-(1) Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, kwa minajili ya sheria zitumikazo sehemu zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(2) Vifungu vya Sheria hii vitatumika katika, na kuhusiana na Sheria yoyote iliyotungwa, nyaraka za umma, hata kama sheria na nyaraka hizo zimetungwa, kupitishwa au kutolewa kabla au baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, isipokuwa kama Sheria na nyaraka hizo:–

(a) Zitakuwa na vifungu vinavyoelekeza vinginevyo, na kuhusiana na sheria, dhamira na malengo yake au maudhui, muktadha au mazingira ya sheria hiyo hayaruhusu, au sheria yenyewe imetoa ufafanuzi;

(b) zinahusu sheria ndogo, kama madhumuni na malengo ya sheria kuu ambayo chini yake sheria ndogo zimetungwa, haziruhusu matumizi ya ufafanuzi huo; au

(c) Zinahusu sheria ndogo, kama madhumuni na malengo ya sheria kuu ambayo sheria ndogo zimetungwa, hayapatani na matumizi ya ufafanuzi huo.

(3) Vifungu vya Sheria hii vitatumika katika Sheria hii kama vitumikavyo katika sheria iliyotungwa baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

(4) Katika vifungu 13, 15, 19, 20, 22, 23, 24, 33, 36(6), 43, 46, au 62 marejeo katika sheria yoyote au sheria ndogo iliyopitishwa au kutungwa baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii yatatafsiriwa ili yasiwe na maana ya kugusa sheria yoyote ambayo inaendelea kutumika au ambayo inarekebisha moja kwa moja sheria nyingine, lakini haibatilishi au kufuta sheria iliyopo.

Jamhuri kufungwa na sheria

3. Jamhuri kufungwa na sheria.

SEHEMU YA PILI
MASHARTI YA JUMLA YA TAFSIRI

Ufafanuzi utumikao katika sheria, Sura ya 16.

4. Katika Sheria hii na katika sheria zingine:–

"shiriki kutenda jinai" kwa maana ya maneno yenye asili hii au misemo inayoshabihiana itakuwa na maana kama ilivyoainishwa katika sheria ya Kanuni za Adhabu;

"tendo" ikitumiwa kuainisha kosa la jinai au kosa la madai itajumuisha kushindwa kutenda wajibu na itahusu msururu wa vitendo vya kushindwa kutekeleza wajibu;

"Sheria" itumikapo kuhusiana na sheria yoyote, itakuwa na maana ya sheria za zamani, amri au sheria zilizotungwa na Bunge la Jamhuri au Baraza la Wakilishi la Zanzibar au Baraza lolote lenye mamlaka ya kutunga sheria Tanzania au kuhusiana na Zanzibar, sheria, amri au sheria za zamani zilizoridhiwa na au kwa niaba ya Rais au mamlaka yoyote ya kutunga sheria, lakini haitahusu sheria ya Jumuiya;

"afisa tawala" maana yake ni afisa tawala wa ngazi yoyote;

"wakili" maana yake ni mtu yeyote anayeruhusiwa kuendesha shughuli za uwakili katika Mahakama Kuu au Mahakama za chini yake, kwa mujibu wa sheria inayohusu uratibu wa shughuli za mawakili;

"hati ya kiapo" kuhusiana na watu wanaoruhusiwa kushuhudia viapo au kupokea ushuhuda badala ya kiapo, itahusu vile vile tamko la dhati, uthibitisho au azimio;

"rekebisha au batilisha" maana yake ni kubadilisha, kufuta au kurekebisha sehemu yote au sehemu tu, au kuongeza au kupunguza au kufanya aina yoyote ya marekebisho kwenye sheria au sehemu yake;

"sheria ya mapokeo" maana yake ni Sheria yoyote ya India au Sheria ya

Uingereza, ikijumuisha Amri za Baraza la Kifalme ambayo katika wakati huu inatumika Tanzania;

"sheria ndogo" maana yake ni sheria ndogo iliyotungwa kwa mujibu wa sheria kuu;

"mwezi" maana yake ni kipindi kuanzia siku ya kwanza ya mwezi hadi siku ya mwisho ya mwezi husika;

"mwaka" maana yake ni kipindi kuanzia siku ya kwanza ya mwezi wa Januari hadi siku ya thelathini na moja ya mwezi wa Desemba ya mwaka husika;

"sura", "sehemu", "kifungu" na "Nyongeza" maana yake ni sura, sehemu, kifungu na Nyongeza ya sheria husika na "kifungu kidogo" maana yake ni kifungu kidogo cha kifungu ambamo neno hilo limetumika;

"Katibu Mkuu Kiongozi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu kwenye Ofisi ya Rais;

"hakimu" maana yake ni hakimu mkazi, hakimu wa wilaya, hakimu wa mahakama ya mwanzo na maelezo mengine yoyote kuhusu hakimu yaliyotolewa chini ya Sheria ya Mahakama za Mahakimu;

"sarafu" maana yake ni kipande cha chuma cha aina yoyote, kiwe chuma cha thamani au kisicho cha thamani na ambacho kwa wakati husika, kinatumika kama fedha halali ya Jamhuri ya Muungano;

"mwanzo wa kutumika" itumikapo kuhusiana na sheria maana yake ni wakati ambapo sheria husika itaanza kutumika;

"sheria zisizoandikwa" maana yake ni sheria zisizoandikwa za Uingereza;

"Jumuiya ya Madola" maana yake ni mfungamano wa nchi za Madola na nchi tegemezi ndani ya Jumuiya; na "mwanachama wa Jumuiya" au "nchi ya Jumuiya in maana ya Jamhuri ya Muungano na nchi zilizoorodheshwa katika Nyongeza ya Sheria hii;

"Jumuiya" maana yake ni Jumiya ya Afrika ya Mashariki iliyoundwa chini ya Mkataba wa Jumuiya;

"Mfuko Mkuu wa Hazina" maana yake ni Mfuko Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya Mwaka 1977 iliyotungwa na Bunge Maalumu la Jamhuri ya Muungano;

Sura ya 2

"vunja" itumikapo kuhusiana na matakwa au wajibu kisheria au ruhusa au idhini, hakimiliki, leseni au mamlaka kwa mujibu wa sheria itajumuisha vile vile kushindwa kutii masharti au maelekezo ya sheria;

"mahakama" maana yake ni mahakama yoyote yenye mamlaka katika Jamhuri ya Muungano;

"Mhakama ya Rufaa" maana yake ni mahakama inyosikiliza rufaa zote zikatwazo kwa mujibu wa Sehemu ya Pili ya Sheria ya Mamlaka ya Mahakama ya Rufaa;

Sura ya 141

"Wakala wa Mfalme" maana yake ni watu kwa wakati huu wanafanya kazi kama Wakala wa Mfalme kwa Serikali na Utawala wa kigeni

au yeyote wa namna hiyo;

"Sheria ya Kimila" maana yake ni kanuni au mfungamano wa kanuni ambazo zinaainisha haki na wajibu, na ambazo zinatokana na mazoea, kurithiwa au kutungwa, na zinakubaliwa na Jamii ya Kiafrika nchini Tanzania na zenye nguvu ya kisheria, ikijumuisha matangazo ya kanuni mpya au marekebisho yake yanayotungwa chini ya kifungu cha 12 cha sheria ya Usimamiaji wa Haki na Matumizi ya Sheria, na marejeo kwa, "Sheria za Jadi" au Sheria za Jadi na Mila zitakuwa na tafsiri sawa;

Sura ya 358

"ufafanuzi" maana yake ni ufafanuzi uliotolewa kwa mujibu wa sheria ukitoa maana kwa neno au msemo;

"Naibu Waziri" maana yake ni Naibu wa Waziri aliyeteuliwa kwa mujibu wa Ibara ya 55 ya Katiba;

"Wilaya" maana yake ni sehemu yoyote ya Jamhuri iliyotangazwa au kubainishwa hivyo kwa mujibu wa Ibara ya 2 (2) ya Katiba;

"hakimu wa wilaya" inajumuisha hakimu mkazi;

"Hati" inajumuisha chapisho la aina yoyote, waraka wa maandishi ya aina yoyote, yaliyoandikwa au kuelezwa kwenye kitu chochote kwa herufi, tarakimu alama kwa namna moja zaidi ya hizo zilizotajwa, kwa madhumuni ya kutumiwa kwa lengo la kuweka kumbukumbu ndani au juu yake;

"Mamlaka ya Afrika ya Mashariki" maana yake ni Mamlaka ya Afrika ya Mashariki iliyoundwa chini ya Mkataba husika;

"sheria iliyotungwa" maana yake ni sheria iliyotungwa au sehemu ya sheria husika;

"shamba", ikitumika kuhusiana na ardhi, itajumuisha vile vile haki ya kisheria au maslahi, maslahi ya haki, haki ya njia katika ardhi, hakimiliki, dai, dai la kumiliki hadi deni lilipwe, au zuio juu ya miliki ya ardhi;

"mwaka wa fedha" maana yake ni kipindi cha miezi 12 kinachoishia tarehe 30 Juni;

"Afisa Mambo ya Nje" maana yake ni afisa aliyeteuliwa au anayekaimu nafasi ya Afisa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Muungano;

"shughuli/kazi" itajumuisha mamlaka, kazi, wajibu, uwezo wa kisheria na mamlaka ya kisheria;

"*Gazeti*" au "*Gazeti la Serikali*" maana yake ni *Gazeti* linalopigwa chapa na kutangazwa na Mpiga Chapa wa Serikali ya Jamhuri kwa amri ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na inajumuisha nyongeza zake na toleo Maalum la Gazeti hilo;

"Taarifa ya Kawaida" maana yake ni tangazo lisilohusiana na utungwaji wa sheria lililochapishwa katika *Gazeti* au kwa idhini ya Rais au Waziri;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano;

"Mkemia Mkuu wa Serikali" inajumuisha msaidizi wake au mkemia yeyote aliyeajiriwa na Serikali;

"Tangazo la Serikali" maana yake ni sheria ndogo iliyotungwa na Rais,

Waziri au afisa wa serikali au mamlaka yoyote yenye uwezo kutunga sheria ndogo kwa mujibu wa sheria husika;

"Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali" maana yake ni Mpiga Chapa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na mpiga chapa yeyote aliyeidhinishwa kuchapa sheria na nyaraka zingine za Serikali;

"Kamisheni" maana yake ni Kamisheni ya Afrika ya Mashariki iliyoundwa kwa Maagizo ya Mfalme ya Kuanzishwa kwa Kamisheni ya Afrika ya Mashariki, kati ya miaka ya 1947 na 1961 na rejeo katika sheria yoyote kuhusu Kamisheni yatafafanuliwa kama ifuatavyo:–

(a) kwa kipindi ambacho Sheria ya Mkataba wa Uendelezaji wa Huduma za Pamoja katika Afrika ya Mashariki ilikuwa ikitumika, kipindi hicho kitafafanuliwa kama Mfumo wa Huduma za Pamoja;

(b) kwa kipindi baada ya kufutwa kwa Sheria iliyounda Kamisheni, kitafafanuliwa kama kipindi cha Jumuiya;

"Mahakama Kuu" maana yake ni Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Mahakama Kuu ya Zanzibar;

"Sheria za Kifalme" maana yake ni Sheria zilizotungwa na Bunge la Ufalme wa Uingereza;

"mtu binafsi" maana yake ni mtu mmoja;

"Jaji" maana yake ni Jaji wa Mahakama Kuu na inajumuisha vile vile Naibu Jaji;

"mlinzi wa amani" maana yake ni mtu mwenye mamlaka ya kutunza amani;

"ardhi" inajumuisha majengo na aina nyingine ya majengo, na iliyofunikwa na maji, milki yoyote, maslahi, haki ya kutumia njia na haki ya vilivyomo juu au chini ya ardhi husika;

"Afisa Sheria" maana yake ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali na afisa mwingine mzoefu kwenye taaluma ya sheria katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuanzia ngazi ya Wakili wa Serikali Mkuu Mwandamizi au Mwandishi wa Sheria Mkuu Mwandamizi;

"mamlaka ya serikali za mtaa" maana yake ni–

(a) baraza la kijiji, kitongoji, mji, wilaya au mamlaka yoyote ya serikali ya mtaa iliyoundwa chini ya sheria ya Serikali za Mtaa na Mamlaka ya Wilaya; au

Sura ya 287

(b) katika sehemu za mji, ni baraza la mtaa, mji, manispaa au baraza la Jiji liloundwa chini ya Sheria ya Serikali za Mtaa (Mjini);

Suraya .288

"hakimu" maana yake ni hakimu mkazi, hakimu wa wilaya hakimu wa mahakama ya mwanzo na mwingine yeyote aliyeteuliwa kama hakimu kwa mujibu wa Sheria ya Mahakimu;

Sura ya 11

"ndoa" maana yake ni ndoa iliyofungwa na inayotambuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Ndoa, na neno “mume”, “mke” au “mwanandoa” litafafanuliwa kutokana na neno la msingi la aliyeoa au kuolewa;

Sura ya 29

"Waziri" ina maana kama ilivyofafanuliwa katika kifungu cha 9 cha sheria hii na vile vile itajumuisha Makamu wa Rais, Waziri Mkuu; na Waziri maana yake ni waziri mwenye dhamana ya kusimamia shughuli husika na itajumuisha Naibu Waziri kwa wakati huu anayetekeleza kazi za Waziri au kama hakuna waziri wa kusimamia jambo husika, maana yake ni Rais;

"mtoto" maana yake ni mtu ambaye hajafikia umri wa miaka kumi na minane, na neno “mtoto” na mtoto mchanga” yatafafanuliwa kwa maana hiyo;

"mwezi" maana yake ni mwezi katika mwaka, isipokuwa kama neno la sayari limeongezwa ikimaanisha mwezi wa sayari; hivyo, mwezi ukitajwa kuanza au kuhesabiwa katika tarehe isiyokuwa ya kwanza ya mwezi husika, basi mwezi utatimia katika siku ya pili ya tarehe ya mwezi unaofuata, hata kama kipindi husika kinajumuisha siku nyingi au pungufu ya siku thelathini;

"mwenyeji " maana yake ni mtu yeyote mwenye asili ya Kiafrika;

"kiapo" na "hati ya kiapo", anayetakiwa au anayeruhusiwa kuthibitisha bila ya kula kiapo, inajumuisha tamko la dhati na azimio, na “kuapa”, itajumuisha “tamka kwa dhati” na “azimia”;

"Sheria ya zamani" inajumuisha sheria ya ina yoyote, tangazo la kisheria au sheria iliyotungwa au kutolewa kabla ya Amri ya Kifalme kuhusu Tanganyika ya mwaka 1920, na iliyoidhinishwa na Amri hiyo ya Baraza la Kifalme, na sheria ndogo zilizotungwa na kuidhinishwa kutumika chini ya Amri hiyo ya Kifalme, na (isipokuwa ufafanuzi wa neno “Sheria” na “Bunge” katika kifungu hiki) itajumuisha Sheria ya Bunge na sheria ndogo zilizotungwa chini ya sheria husika;

"Bunge":-

(a) katika Sheria za zamani, au katika nyaraka za serikali zilizotolewa au kutangazwa kabla ya tarehe tisa, Desemba, 1961, ina maana ya Bunge la Uingereza na “Bunge la Mfalme” ina maana kama hiyo;

(b) katika sheria za Bunge la Tanganyika au za Bunge la Jamhuri ya Muungano, au nyaraka za Serikali iliyotungwa au kutolewa baada ya siku ya nane, ya Desemba, 1961, au sheria ya Bunge Maalum la Tanganyika itakuwa na maana ya Bunge le Jamhuri ya Muungano (na matumizi ya neno “Sheria ya Bunge” yatajumuisha sheria iliyotungwa na Bunge Maalum la Tanganyika);

"tekeleza" itumikapo kuhusiana na kazi au shughuli, itajumuisha vile vile kutumia uwezo uliotolewa kisheria, kutekeleza wajibu au mamlaka ya kisheria;

"Katibu Mkuu" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Rais kushika wadhifa wa Katibu Mkuu;

“mtu" maana yake ni neno au msemo utumikao kuelezea mtu binafsi au kampuni, shirika au mamlaka iliyoundwa kisheria, au isiyopewa

hadhi ya nafsi;

"afisa polisi" maana yake ni askari yeyote wa Jeshi la Polisi mwenye cheo cha konstebo au zaidi kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Jeshi la Polisi na Majeshi ya Nyongeza;

Sura ya 322

"uwezo" inajumuisha hadhi, mamlaka au hiari ya kuamua;

"iliyoagizwa au ainishwa" ina maana ya–

(a) iliyoainishwa na au chini ya sharia husika ambapo neno hilo limetumika;

(b) kwa pale litumikapo kurejelea kwenye kitu chochote kilichoainishwa kwenye sheria nyingine ukiacha sheria ambamo neno hilo limetumika, itajumuisha kitu chochote kilichoainishwa ndani ya sheria ndogo iliyotungwa kwa mujibu wa sheria husika;

"Rais" maana yake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano, na inajumuisha mtu yeyote mwenye mamlaka ya kutekeleza majukumu ya Rais kwa mujibu wa kifungu cha 137 cha Katiba;

"Tangazo" maana yake ni tangazo la Rais lililochapishwa katika Gazeti la Serikali;

"Chapisho" maana yake ni:-

(a) maandiko au machapisho ya aina zote;

(b) kumbukumbu ya aina yoyote, kinasa sauti, waya, maandishi ya matundu, filamu ya senema, au vivuli, kumbukumbu zitokanazo na uvumbuzi wowote, zitokanazo kwa njia ya elektronik au umeme, zilizorudufuliwa au kuainishwa na kupelekwa kwa njia hizo;

(c) kitu cha aina yoyote kinachofanana na vile vilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha (b) cha ufafanuzi huu au hata kama haviwiani, vikiwa katika hali ya kuweza kuonekana aidha kwa jinsi vilivyo, maumbile yake au kwa namna yoyote vinaweza kutoa au kurudufu au kunakilisha au kuwasilisha maneno au mawazo; na

(d) kila nakala na rudufisho la chapisho lolote lililoainishwa katika vifungu vidogo vya (a), (b) au (c);

"shirika la umma" maana yake ni kampuni iliyoundwa kwa sheria ya kipekee na si chini ya Sheria ya Makampuni, na inajumuisha shirika dogo la kipekee lililoundwa kwa utaratibu usio chini ya Sheria ya Makampuni;

Sura ya 212

"siku ya mapumziko" maana yake ni siku ambayo imetangazwa kuwa siku ya mapumziko chini ya Sheria ya Siku za Mapumziko;

Sura ya 35

"mtumishi wa umma" au "idara ya umma" inajumuisha kila afisa au idara iliyopewa mamlaka ya kushughulikia mambo ya umma, aidha chini ya maelekezo ya moja kwa moja kutoka kwa Rais au vinginevyo, na inajumuisha afisa au idara chini ya Mamlaka ya Serikali ya Mtaa, Jumuiya au Shirika la Umma;

"sehemu ya wazi au umma" inajumuisha:-

(a) mtaa, barabara, gati au bustani ya umma;

(b) jengo, mahala au chombo kitumikacho kwa usafiri wa umma au ambacho kila mtu anayo haki au anaruhusiwa kukitumia au kuwemo aidha bila ya masharti au kwa masharti au kwa kulipa ada au kiingilio;

(c) jengo au mahala au chombo kitumikacho kwa umma kwa ajili ya shughuli za mikutano ya kidini au mkusanyiko wa watu au kama mahakama;

"mhuri wa umma" maana yake ni mhuri wa Jamhuri ya Muungano;

"Mkoa" maana yake ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano iliyotangazwa au inayofahamika kutolewa Tamko na Rais chini ya Ibara ndogo (2) ya Ibara ya 2 ya Katiba kuwa ni mkoa;

"Mkuu wa Mkoa " maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Rais kuwa mkuu wa mkoa, na "Mkuu wa Mkoa" ni mkuu wa mkoa husika;

"kanuni" maana yake ni kanuni zilizotungwa chini ya sheria ambamo neno hilo limetumika;

"futa au batilisha" inajumuisha kutengua, kubadili, kusawazisha au kufuta;

"Jamhuri" maana yake ni Jamhuri ya Tanganyika na inajumuisha Jamhuri ya Muungano;

Sura ya 11

"hakimu mkazi" maana yake ni hakimu mkazi wa daraja lolote aliyeteuliwa hivyo chini ya Sheria ya Mahakama ya Mahakimu;

"afisa mapato" maana yake ni afisa aliyeteuliwa na Katibu Mkuu wa Hazina kufanya shughuli za kukusanya mapato ya Jamhuri ya Muungano;

"taratibu" maana yake ni, taratibu zilizotungwa chini ya sheria husika ambamo neno hilo limetumika;

"taratibu za mahakama" itumikapo kuhusiana na mahakama, maana yake ni taratibu zilizotungwa na mamlaka yenye uwezo wa kutunga kanuni, kutoa maagizo ya kuratibu utendaji na taratibu za uendeshaji wa shughuli za mahakama;

"uza au kuuza" inajumuisha kubadilishana bidhaa, kutoa kwa ajili ya kuuza na kutandaza bidhaa hadharani kwa ajili ya kuuza;

"wasilisha " pale sheria inaporuhusu au kuhitaji hati yoyote kuwasilishwa kwa mtu yeyote, ikiwa msemo wa "kuwasilisha", au msemo wa "toa" au "peleka" au msemo mwingine wowote ukitumika basi isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo, kuwasilisha kutakamilika kwa kuandika anuani sahihi na kuituma kwa posta, baada ya kulipa tozo husika, barua yenye hati na isipokuwa kama kinyume chake kimedhibitishwa, uwasilishaji utachukuliwa kama umeshawasilishwa katika muda wa kawaida wa huduma za posta;

"saini" ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya kisarufi chake na asili ya msemo wa neno hili, itajumuisha jina au alama, kwa mtu asiyeweza kuandika;

"siku za vikao" likitumika kuhusiana na Bunge, maana yake ni siku ambapo Bunge limekaa;

"tamko la kisheria", kama likitolewa:-

(a) nchini Tanzania, maana yake ni tamko lililofanywa chini ya Sheria ya Viapo na Matamko ya Kisheria;

Sura ya 34

(b) katika nchi nyingine ya Jumuiya ya Madola, maana yake ni tamko chini ya kiapo kilichotolewa mbele ya mlinzi wa amani, mthibitishaji rasmi au mtu mwingine yeyote mwenye mamlaka ya kutoa au tamko kupokea viapo kwa mujibu wa sheria yoyote inayotumika katika nchi hiyo;

(c) katika nchi nyingine yoyote, maana yake tamko chini ya kiapo kilichotolewa mbele ya Afisa wa Mambo ya Nchi za Nje mwenye mamlaka ya chini ya sheria yoyote kuhusu kupokea viapo au mtu mwingine yeyote aliyeteuliwa na kukasimiwa madaraka hayo na Waziri wa Mambo ya nje kwa mujibu wa Tangazo lililochapishwa katika Gazeti la Serikali;

"sheria ndogo" maana yake ni amri, tamko la kisheria, kanuni, kanuni za mahakama, tangazo, sheria ndogo za miji, kijiji au chama au hati ya kisheria iliyotolewa na mamlaka yoyote kwa mujibu wa Sheria husika;

"tia hatiani/papohapo" maana yake ni kutolewa kwa hukumu na mahakama yenye mamlaka ya kutoa hukumu papo hapo;

"apa/apisha" kwa mtu anayeruhusiwa kwa mujibu wa sheria kutoa tamko la dhati au uthibitisho badala ya kiapo, itajumuisha kutoa tamko la dhati kutoa uthibitisho wa dhati;

"maji ya taifa" maana yake ni maji ya bahari, mto au ziwa yaliyopo ndani ya mipaka ya Jamhuri ya Muungano;

"himaya" maana yake ni Tanganyika;

"Mkataba" maana yake ni Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki ulioainishwa katika Nyongeza ya Sheria ya (Kutekeleza) Mkataba wa Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki ya mwaka 1967 ambayo ilifutwa chini ya Sheria ya Mkataba wa Usuluhishi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki;

Sura ya 323

"chini" itumikapo kuhusiana na sheria au kifungu chochote cha sheria, itajumuisha “ya”, “kwa mujibu wa” “kufuatana na” na “kutokana na”;

"Siku ya Muungano" maana yake ni tarehe 26 Aprili, 1964;

"Falme Zilizoungana" maana yake ni Uingereza na Ireland ya Kaskazini;

"Jamhuri ya Muungano" maana yake–

(a) kwa kipindi baada ya terehe 11 Desemba, 1964 ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) kwa kipindi kilichoanzia Siku ya Muungano na kuishia tarehe 11 Desemba, 1964 ni Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar;

"Makamu wa Rais" maana yake ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;

"wosia" inajumuisha sehemu ya wosia, kiambatanisho cha wosia au

kiambatanisho cha wosia kinachotangua sehemu ya wosia;

"maneno" yanajumuisha tarakimu na alama;

"maandiko/maandishi", na maelezo yanayotaja maandiko au maandishi yatajuisha vilevile picha, lithographia, kuandika au kuchora na jiwe na aina zozote za kuonyesha maandiko au kurudufu maneno kwa namna ya kuonekana;

"sheria za Bunge" maana yake ni Sheria zote zilizotungwa na Bunge ambazo kwa wakati husika zinatumika pamoja na sheria ndogo zote zinazotumika zikiwepo na Sheria za Jumuiya pamoja na sheria zote zilizoazimwa;

"mwaka" maana yake ni kipindi cha miezi kumi na miwili.

Matumizi

5. Fasili au kanuni za ufafanuzi zilizomo katika sheria yoyote zitatumika kufafanua vipengele vya sheria ambamo vipo au kanuni za ufafanuzi zilizopo katika sheria hiyo, pamoja na vipengele vingine vya sheria hiyo.

Sheria hunena daima

6. Sheria ya Bunge itachukuliwa kama inanena wakati wote na litokeapo jambo au kitu kimeelezwa katika wakati wa sasa, ifahamike kuwa inajumuisha nyakati zote, ili kila sehemu yoyote ya sheria husika ipewe maana yake halisi kulingana na maudhui na malengo ya sheria husika.

Sehemu ya matamshi na miundo ya fasihi

7. Mahali ambapo neno au fungu la maneno vimefafanuliwa katika sheria, sehemu zingine za msemo au vifungu vya maneno vitakuwa na maana sawia.

Jinsia na tarakimu

8. Katika sheria yoyote:-

(a) maneno yanayoonyesha jinsia ya kiume yatajumuisha vilevile jinsia ya kike;

(b) maneno yanayoonyesha jinsia ya kike yatajumuisha vilevile jinsia ya kiume;

(c) maneno ya umoja yatajumuisha vilevile uwingi na maneno ya uwingi yatajumuisha umoja;

Rejeo ya neno Waziri katika sheria

9. Anapotajwa Waziri katika sheria tafsiri yake itakuwa ni moja ya zifuatazo–

(a) anapotajwa Waziri ndani ya sheria, ifafanuliwe kuwa ndiye waziri mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa sheria hiyo, au kama ni katika vifungu vya sheria ambamo au kwa mujibu wa vifungu hivyo neno hilo limetumika, itakuwa na maana kwamba mwenye dhamana wakati huo ni Rais;

(b) iwapo ni kwenye sheria ndogo, neno waziri mwenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria au vifungu vya sheria, itakuwa na maana mwenye dhamana wakati huo ni Rais; na

(c) itajumuisha Kaimu Waziri badala ya Waziri husika kama ilivyoelekezwa katika kifungu (a) au (b).

Marejeo kwa tarakimu kujumuishwa

10. Rejeo kwenye sheria kwa kutumia namba au herufi au kwa namba na herufi kwa pamoja, au kwa sehemu mbili au zaidi ya sheria husika, itatafsiriwa kama inajumuisha sehemu iliyoelezwa kwa kutumia rejeo iliyofafanuliwa awali na ile iliyorejewa mwishoni.

Tafsiri ya rejeo ndani ya kifungu, n.k.

11.-(1) Endapo katika sheria, rejeo imefanywa kwenye sura, sehemu, nyongeza, kiambatanisho au fomu bila ya maelezo mengine ya kuonyesha rejeo imefanywa kwenye sura, sehemu, kifungu nyongeza, kiambatanisho au fomu ya au kwa mujibu wa sheria nyingine, basi rejeo hiyo itatafsiriwa kana kwamba inahusiana na sheria husika ambamo rejeo limefanywa.

(2) Endapo katika kifungu cha sheria, rejeolimefanywa kwenye kifungu kidogo, aya, aya ndogo, au kipengele chini ya hivyo, na bila ya maelezo mengine ya kuonyesha kama rejeo la kifungu kidogo, aya, aya ndogo au kipengele kidogo chini ya hivyo imefanywa kwa mujibu wa sehemu nyingine au kifungu kingine, basi rejeo hilo litakuwa kwa mujibu wa na itatafsiriwa kana kwamba ni rejeo kwa kifungu kidogo, aya, aya ndogo au sehemu ya kifungu ambamo rejeo hilo limefanyika.

(3) Endapo katika nyongeza ya sheria, rejeo imefanywa kwenye kipengele, aya, au sehemu nyingine bila ya maelezo ya kuonyesha kwa mahsusi, kipengele, kipengele kidogo, aya au sehemu nyingine mahsusi, basi rejeo hilo litakuwa kwa mujibu wa na litatafsiriwa kana kwamba ni rejeo kwenye kipengele, kipengele kidogo, aya, au sehemu nyingine ya nyongeza ambayo rejeo hilo limefanyika.

(4) Masharti ya vifungu (1), (2), na (3) yatatumika baada ya kuzingatia mabadiliko ya lazima kuhusiana na ufafanuzi wa maudhui ya sheria ndogo husika.

Rejeo kwenye sheria kama ilivyorekebishwa

12.-(1) Rejeo katika sheria kwenye sheria nyingine, litachukuliwa kujumuisha rejeo kwenye sharia hiyo kama ilivyorekebishwa.

(2) Rejeo katika sheria kwenye kifungu cha sheria, litatafsiriwa kama rejeo kwenye kifungu husika kama kitakavyorekebishwa.

(3) Rejeo katika sheria kwenye Sheria ya Kifalme, au kwenye kifungu cha Sheria ya Kifalme, litatafsiriwa kujumuisha rejeo kwenye sheria hiyo ya Kifalme au kifungu kama kitakavyorekebishwa.

Tafsiri ya neno "au" kitofauti

13. Kuhusiana na sheria iliyotungwa au kupitishwa baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, lakini kwa kuzingatia kifungu cha 2 (4), "au", "ingine" na "vinginevyo" yatatafsiriwa kuelezea tofauti na sio lazima kuonyesha usawa au uwiano, isipokuwa kama neno "a kufanana" au maneno mengine yenye maana hiyo yameongezwa.

SEHEMU YA TATU
KUANZA KUTUMIKA NA KUTAJWA KWA SHERIA

Tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria

14. Kila sheria itaanza kutumika katika tarehe ya kuchapishwa kwake katika Gazeti la Serikali, isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo au kama imeelekezwa katika sheria husika au katika sheria nyingine kwamba sheria hiyo itaanza kutumika katika tarehe nyingine.

Muda wa kuanza kutumika kwa sheria

15. Ikielekezwa kwamba sheria itaanza kutumika siku Fulani, basi sheria hiyo itaanza kutumika kuanzia alfajiri ya siku hiyo.

Kuanza kutumika kwa sheria palipo na kifungu cha masharti ya kutolewa taarifa ya kuanza kutumika

16. Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 14, kwa pale ambapo sheria imeelekeza au kifungu cha sheria hiyo kimeelekeza kuwa sheria itaanza kutumika katika tarehe itakayoteuliwa kwenye tangazo, kifungu hicho na kile kinachotoa jina la sheria, vitaanza kutumika tarehe Sheria inaposainiwa na Rais, isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo.

Tafsiri ya uwezo wa kupanga siku ya kuanza kutumika kwa sheria

17. Uwezo wa kutangaza siku ya kuanza kutumika kwa sheria haujumuishi uwezo wa kuainisha au kutangaza-

(a) siku ya nyuma kabla ya tarehe ambapo tangazo hilo linachapishwa katika Gazeti la Serikali; au

(b) siku tofauti kwa vifungu tofauti vya sheria hiyo, isipokuwa kama kuna vifungu dhahiri vinavyoruhusu kufanya hivyo.

Ushahidi wa tarehe ya kusainiwa

18. Pale ambapo inaonekana tarehe katika nakala ya Sheria iliyochapishwa, au inayodaiwa kuchapishwa na Mchapa Mkuu wa Serikali, ikionyeesha kuwa ndiyo tarehe ambapo Rais aliridhia na kusaini Sheria hiyo au sehemu yake, tarehe hiyo inayoonekana ndiyo itakayochukuliwa kama ushahidi kuwa siku hiyo ndiyo ambamo Rais aliweka saini yake katika Sheria hiyo, na mahakama zitaridhia hivyo.

Utekelezaji wa uwezo kabla ya kuanza kutumika

19.-(1) Endapo kifungu cha sheria hakianzi kutumika baada ya kutungwa kwa sheria husika na kifungu hicho kama kingeanza kutumika kingeweza kutoa mamlaka ya–

(a) kutolewa hati/agizo la kisheria au kiutawala;

(b) kutoa notisi au hati ya aina nyingine;

(c) kuteua mtu kushika madaraka fulani;

(d) kuanzisha mamlaka inayoundwa na watu fulani, mamlaka ambayo ni ya kisheria au siyo ya kisheria, au

(e) kufanya jambo lolote kwa mujibu wa sheria hiyo;

Basi, uwezo huo wa kisheria, bila ya kujali kwamba kifungu hicho hakijaanza kutumika, lakini kwa kuzingatia masharti ya vifungu vya (3) na (4), uwezo huo waweza kutumika wakati wowote baada ya kutungwa kwa sheria hiyo kwa jinsi ikatavyoonekana ni lazima au ni muhimu kwa lengo la kuwezesha sheria hiyo au vifungu vyake kuanza kutumika, au

vifungu vyake kutumika mara baada vifungu hivyo kuanza kutumika.

-(2) Kwa pale ambapo–

(a) kifungu cha sheria hakianzi kutumika baada ya kutungwa kwa sheria na kifungu hicho kingerekebisha Sheria kama kingeanza kutumika;

(b) kifungu cha ile sheria nyingine kingeweza, kama kifungu kilichotajwa awali kingeanza kutumika kutoa uwezo wa–

(i) kutoa amri au hati yenye nguvu kisheria au kiutawala;

(ii) kutoa notisi au hati ya aina nyingine;

(iii) kuteua mtu kushika wadhfa au madaraka ya ofisi fulani;

(iv) kuunda chombo maalumu chenye au kisichokuwa na taaswira ya kampuni; au

(v) kufanya jambo lolote kwa madhumuni ya ile sheria nyingine,

basi, uwezo huo, bila ya kujali kuwa kifungu kilichotajwa awali hakijaanza kutumika, lakini kwa kuzingatia matakwa ya vifungu vya (3) na (4) vyaweza kutumika wakati wowote baada ya kupitishwa kwa sheria ambamo kifungu kilichotajwa awali kimo, na kwa jinsi ilivyo lazima au muhimu kwa lengo la kuwezesha ile sheria nyingine iweze kutumika au vipengele vya sheria ile, mnamo au baada ya kifungu kilichotajwa awali kuanza kutumika.

-(3) Kwa pale ambapo uwezo wa kutoa hati au amri zenye nguvu kisheria au kiutawala upo, au uwezo wa kutoa notisi au hati nyingine, uwezo huo waweza kutumiwa kama ilivyoelekezwa katika kifungu kidogo cha (1) au cha (2), na hati hiyo, au notisi yaweza kuwa na nguvu/kuanza kutumika:-

(a) katika siku ambayo sharti lililorejewa katika kifungu kidogo cha (1) au, kama itakavyokuwa, sharti lililotajwa mwanzo katika kifungu kidogo cha (2) kinaanza kutumika; au

(b) katika siku ambayo kingeanza kutumika, iwapo muda ule ambapo hati ilipotolewa, au notisi au waraka , kifungu kilichotajwa au kilichotajwa awali kitakuwa kimeanza kutumika, kutegemea na kitakachotokea mwishoni.

-(4) Pale uwezo wa kuteua mtu katika ofisi fulani, au kuunda taasisi unatekelezwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) au cha (2), mtu aliyeteuliwa kushika wadhifa huo anaweza kutekeleza majukumu ya ofisi hiyo, au vyovyote itakavyokuwa, taasisi iliyoundwa inaweza kukutana na kutekeleza kazi, wajibu na uwezo, lakini tu kwa kuzingatia madhumuni yaliyorejewa katika kifungu kidogo cha (1) au cha (2) kutegemeana na kifungu kidogo kitakachotumika; na kwa madhumuni ya kifungu chochote kinachohusu muda, kitachukuliwa kutokuanza mpaka kifungu husika kilichorejewa katika kifungu cha (1) au cha (2) kwa vyovyote itakavyokuwa, kuanza kutumika.

(5) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (4) cha

kifungu cha (2), kifungu hiki kitatumika katika sheria zilizopitishwa baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Kutajwa kwa Sheria

20.-(1) Pale sheria imerejewa, itakuwa inatosheleza kwa madhumuni yote kutaja au kurejea sheria hiyo kwa:-

(a) jina fupi au mtajo (kama upo) kwa jinsi ambavyo sheria hiyo imetajwa;

(b) kama ni sheria, mwaka ilipopitishwa na namba yake kati ya sheria nyingine za mwaka huo;

(c) kama ni sheria, namba ya Sura ya sheria hiyo katika Juzuu za sheria zilizorekebishwa.

(2) Kifungu cha sheria kinaweza kutajwa kwa rejeo la sehemu, kifungu, kanuni, taratibu, ibara au mgawanyo wowote wa sheria ambapo kifungu hicho kinapatikana.

(3) Mtajo wa sheria yoyote utafanywa kutegemeana na nakala ya chapisho la sheria, au chapisho linalodhaniwa kuwa limechapwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

Marejeo ya sheria kwa siku ya kuanza kutumika

21. Rejeo la sheria kuhusu siku ya kuanza kutumika itakuwa, pale, baadhi ya vifungu vinaanza kutumika katika tarehe tofauti, itakuwa siku ile ambayo kifungu husika cha sheria hiyo kinaanza kutumika.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA UTUNGWAJI WA SHERIA NA UTUMIKAJI WA SHERIA

Sheria kuwa sheria ya Umma

22. Kila sheria itahesabiwa kuwa iko wazi na inafahamika kwa umma wote, isipokuwa kama kutakuwa na maelezo ya kuonyesha vinginevyo, na mahakama zote zitatilia maanani kuwa sheria zote zinafahamika kwa umma.

Vifungu kujitosheleza kama sheria kamili

23. Kila kifungu cha sheria kitakuwa na maana na uwezo timilifu kama sheria bila ya kuwa na haja ya / ulazima wa maelezo ya utangulizi / dibaji.

Kifungu kinaweza kurukwa au kufutwa katika Kikao hicho hicho

24. Sheria inaweza kurekebishwa au kufutwa katika kikao hicho hicho cha Bunge kama kile kilichopitisha sheria hiyo.

Utangulizi na Majedwali

25.-(1) Utangulizi katika sheria, ni sehemu ya sheria husika, na unapaswa kutafasiriwa kama sheria yenyewe, kwa madhumuni ya kusaidia kutoa ufafanuzi na madhumuni ya sheria hiyo.

(2) Kiambatanisho au Jedwali au orodha katika sheria pamoja na maelezo mafupi vitakuwa ni sehemu ya sheria hiyo.

Vichwa, maelezo

26.-(1) Vichwa vya habari ya sehemu, mgawanyo na sehemu ya

ya pembeni, na marejeo chini ya ukurasa na marekebisho makosa ya Na 17 ya 1996 Jedwali.

mgawanyo vitahesabika kama sehemu ya sheria hiyo.

(2) Maelezo ya pembeni au rejeo za chini ya kurasa katika sheria, na bila ya kuathiri kifungu cha (1), kichwa cha sehemu ya sheria, kanuni, taratibu sheria-ndogo au ibara ya sheria havitahesabika, kama sehemu ya sheria.

(3) Ikiwa kutakuwa na kosa lolote la maandishi au uchapishaji wa Muswada wa Sheria au Sheria yenyewe kwenye *Gazeti la Serikali,* Mwandishi Mkuu wa Sheria au afisa yeyote wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali aliyepewa madaraka kwa maandishi kwa niaba hiyo na Mwandishi Mkuu wa Sheria anaweza kwa amri iliyochapishwa katika gazeti la Serikali kutoa maelekezo ya kusahihisha makosa hayo na kila agizo litasomeka pamoja na Muswada au Sheria inayohusiana nayo na Mswada huo au Sheria, kuanzia tarehe ya kuchapishwa itaanza kutumika kama ilivyosahihishwa.

SEHEMU YA TANO
MAREKEBISHO NA KUFUTWA KWA SHERIA

Fasiri ya sheria inayorekebisha Sheria pamoja na marekebisho yake

27. Pale ambapo sheria inarekebisha sheria nyingine, marekebisho ya Sheria hiyo, kama yatakuwa yamebeba maudhui ya Sheria inayorekebishwa bila ya kuwa na madhumuni mengine, itafafanuliwa na kufasiriwa kama sehemu ya Sheria iliyorekebishwa.

Kufutwa kwa Sheria kama ilivyorekebishwa

28. Pale ambapo Sheria iliyorekebishwa kwa Sheria nyingine imefutwa, kufutwa kwa Sheria hiyo kutahusu pia kufutwa kwa vipengele vyote vya ile Sheria ya mwanzo ambayo ilirekebishwa.

Kufuta kwa kufuta

29. Pale ambapo Sheria inafuta Sheria inayorekebisha, kufuta huko hakutahuisha sheria yoyote ambayo ilikuwa imefutwa, isipokuwa kama yameongezwa maneno ya kuhuisha sheria hiyo.

Kufuta na Kubadilisha

30. Pale ambapo Sheria inarekebisha Sheria nyingine na kuweka vifungu vingine mbadala, Sheria iliyorekebishwa itabakia hai na itaendelea kutumika hadi hapo vifungu vilivyowekwa mbadala vitakapoanza kutumika.

Amri ya masharti mbadala

31. Pale ambapo Sheria inarekebisha na inatunga sheria nyingine pamoja na au bila ya mabadiliko, katika sheria yoyote iliyotungwa:-

(a) wilaya zote au mgawanyo wa maeneo mengine;
(b) halmashauri zote, mashirika, bodi, mabaraza, kamisheni, bodi za wadhamini au mamlaka zingine zilizoundwa na chaguzi zote na uteuzi wowote uliofanywa; na
(c) ofisi zote zilizoanzishwa na uteuzi wowote wa maafisa uliofanywa;
(d) sheria ndogo zote, hati, vyeti na nyaraka zilizotolewa; na
(e) matendo mengine yote, mambo na vitu,

ambavyo wakati sheria inayofuta inaanza kutumika yalikuwepo, au yalikuwa na nguvu kisheria, kwa mujibu wa vifungu vya sheria hiyo, yataendelea kuwa halali kama kwa mujibu wa vifungu hivyo yanaruhusiwa kuendelea, au yamehuishwa, yamefanywa au kutendwa na yamechimbuka au kuhalalishwa au kutendwa kwa mujibu wa sheria hiyo.

Vifungu vya jumla vinavyobakizwa baada ya kufutwa

32.-(1) Pale ambapo Sheria inafuta au kurekebisha Sheria nyingine, sheria iliyofutwa, isipokuwa kama kuna madhumuni tofauti-

(a) haitahuisha jambo lolote ambalo halikutumika au halikuwepo wakati ufutwaji unaanza kutumika;
(b) hautaathiri matumizi yaliyopita ya sheria iliyofutwa au kitu chochote kilichofanywa kwa usahihi kuhamishwa chini ya sheria hiyo;
(c) haitaathiri haki yoyote, maslahi, hatimiliki, uwezo, upendeleo uliotolewa, uliopatikana, uliojitokeza, ulioanzishwa au uliotekelezwa au hadhi yoyote au uwezo kabla ya ufutwaji;
(d) haitaathiri wajibu wowote, shuruti, kuwiwa au wajibu wa kuthibitisha uliotwikwa, uliotolewa au ulioingiwa;
(e) haitaathiri utwaaji adhabu au utwaaji ulioingiwa au wajibu wa kuingiwa kutokana na kosa lililotendwa dhidi ya sheria hiyo;
(f) haitaathiri uchunguzi wowote, mwenendo wa kisheria au nafuu kuhusiana na haki yoyote, maslahi, hakimiliki, uwezo, hadhi, wajibu, shuruti au wajibu wa kuthibitisha, adhabu au kutwaliwa kwa mali;

na uchunguzi wowote, mwenendo wa kisheria au unafuu unaweza kuanzishwa, kuendelezwa au kutekelezwa na adhabu yoyote hiyo au utwaaji unaweza kutwikwa na kutekelezwa kama vile sheria inayofutwa hayapitishwa au kutolewa.

(2) Kuwepo kwa vifungu vinavyobakizwa dhahiri kuhusiana na kufutwa kulikofanyika hakutachukuliwa kuathiri matumizi ya kifungu hiki kuhusiana na athari ya kufutwa kulikofanyika.

Athari ya kufutwa kwa sheria kwenye sheria ndogo

33.-(1) Pale ambapo sheria:-

(a) inafuta au kurekebisha sheria nyingine na kuweka vifungu mbadala au ;
(b) inafuta na kutunga sheria nyingine bila ya au pamoja na marekebisho,

Sheria ndogo zote zilizotungwa chini ya Sheria inayofutwa na ambazo zilikuwa zinatumika kabla ya kuanza kutumika kwa sheria inayofuta sheria nyingine, kama zinzenda sambamba na Sheria inayofuta Sheria nyingine, zitaendelea kutumika na kuwa na nguvu kisheria kana kwamba sheria ndogo hizo zimetungwa chini ya Sheria inayofuta sheria nyingine..

(2) Sheria ndogo inayoendelea kutumika chini ya kifungu kidogo cha (1), inaweza kurekebishwa au kufutwa kama vile imetungwa chini ya

Sheria inayofuta sheria nyingine.

Athari ya kumalizika kwa muda wa kutumika kwa sheria

34. Mara baada ya muda wa kutumika kwa Sheria utakapoisha, au kutumika kwa Sheria kutakapofikia tamati, kifungu cha 33 kitatumika kama vile Sheria iliyotungwa itakuwa imefutwa .

SEHEMU YA SITA
MASHARTI YANAYOHUSU SHERIA NDOGO

Rais anaweza kutunga Sheria Ndogo

35. Iwapo sheria yoyote inaruhusu au imeweka masharti ya kutungwa kwa sheria ndogo na haielekezi ni nani mwenye mamlaka ya kutunga sheria ndogo hizo, basi ndogo hizo zinaweza kutungwa na Rais.

Masharti ya jumla kuhusu uwezo wa kutunga Sheria Ndogo

36.-(1) Sheria ndogo haitakuwa kinyume na masharti ya Sheria Kuu ambayo imetoa mamlaka ya kutungwa kwa, Sheria Ndogo hiyo, au sheria nyingine, na Sheria Ndogo itakuwa batili kwa kiasi ilivyokuwa kinyume na matakwa ya Sheria Kuu.

(2) Pale Sheria Ndogo inaelekea kutungwa kwa kutekeleza mamlaka fulani au mamlaka nyingine, itachukuliwa kuwa imetungwa kwa kutekeleza mamlaka zote ambazo zimepelekea kutungwa kwa Sheria hiyo .

(3) Itachukuliwa kwamba panapokuwa hakuna ushahidi vinginevyo, masharti yote na hatua za mwanzo muhimu ya kutungwa kwa Sheria Ndogo zitakuwa zimefuatwa na kufanywa.

(4) Pale Sheria inatoa uwezo wa kutunga Sheria Ndogo, itachukuliwa kwamba imejumuisha mamlaka ya kutekeleza kwa utaratibu kwa namna hiyo na kwa mujibu wa masharti (kama yatakuwepo) ya kurekebisha au kufuta Sheria Ndogo yoyote; na kama mtu aliyepewa mamlaka hayo atakuwa amebadilishwa kabisa au kupewa mtu mwingine, uwezo uliotolewa chini ya kifungu kidogo hiki, juu ya mtu wa mwanzo unaweza ukafanywa na mtu aliyebadilishwa juu ya mambo yote au vitu ambavyo viko chini ya mamlaka yake kama vile ni mtu wa mwanzo

(5) Pale ambapo Sheria inampa uwezo mtu wa kutunga Sheria Ndogo kwa madhumuni ya jumla na pia kwa madhumuni yoyote maalum yanayohusiana na maudhui hayo, kutajwa kwa madhumuni maalum hakutaathiri ujumla wa mamlaka au uwezo wa kutunga Sheria kwa madhumuni ya jumla yaliyoainishwa.

(6) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) cha Kifungu cha 2, Sheria Ndogo inaweza kuweka masharti kwamba kukiukwa kwa sheria ndogo ni kosa linaloweza kuadhibiwa kwa kutozwa faini kuhusiana na kosa hilo kwa kiwango kisichozidi shilingi laki sita.

(7) Uwezo wa kutunga Sheria Ndogo unaweza ukafanywa–

(a) ama kuhusiana na jambo lolote ambalo uwezo huo umetolewa, au kuhusiana na mambo yote ambayo yametolewa maelezo maalum, au kuhusiana na jambo maalum au mambo yaliyoainishwa; na

(b) kwa ajili ya kuweka, kwa ajili ya mambo ambayo yanatekelezeka –

(i) sharti sawa kwa mambo yote yanayohusu uwezo unaotekelezwa au kifungu tofauti kwa mambo tofauti au aina au mambo au masharti tofauti kwa jambo linalofanana au aina mbalimbali ya mambo kwa madhumuni tofauti ya sheria; au

(ii) sharti jingine lolote ama bila masharti au kwa sharti lolote maalum.

(8) Sheria Ndogo inaweza kutungwa–

(a) kwa ajili ya kutumika–

(i) muda wote au muda maalum;

(ii) wakati wote au katika sehemu maalumu ya;

(b) kwa ajili ya kuhitaji jambo lolote litakalokuwa limeathiriwa na sheria kuwa–

(i) kwa mujibu wa viwango maalum au matakwa maalum;

(ii) iliyoidhinishwa na au kwa kuridhika kwa mtu maalum au chombo au aina ya watu maalum au chombo;

(c) kwa ajili ya kumpa mamlaka ya ridhaa kwa mtu maalum au chombo au aina maalum ya watu au chombo; na

(d) kwa ajili ya kutoa katika jambo maalum au aina ya mambo kwa ajili ya kutoa watu au vitu au aina ya watu au vitu kutoka kwenye masharti ya sheria ndogo ama kwa masharti maalum ama vyote au kwa kiwango maalum kilichoelezwa.

(9) Kwenye vifungu vidogo vya (7) na (8), neno "Maalum" maana yake maalum kwenye Sheria Ndogo.

Utangazaji na kuanza kutumika kwa Sheria Ndogo

37.-(1) Pale Sheria inapotoa mamlaka ya kutunga Sheria Ndogo, Sheria Ndogo zote zilizotungwa chini ya mamlaka hiyo isipokuwa kama nia iliyokinyume inajitokeza –

(a) inatangazwa kwenye Gazeti la Serikali;

(b) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) na kifungu cha 39,, itaanza kutumika siku ya kutangazwa, au pale siku nyingine maalum itakapotamkwa au kutolewa katika Sheria Ndogo kwenye siku hiyo.

(2) Sheria Ndogo haitatamka kuanza kutumika katika siku kabla ya siku ya kutangazwa, pale inapotokea iwapo Sheria Ndogo imeanza kutumika:-

(a) haki ya mtu yeyote (ambaye si Serikali au taasisi ya serikali) iliyopo mara kabla ya siku ya utangazaji itaathiriwa kwa namna ambayo itamuathiri mtu huyo; au

(b) wajibu utatwikwa kwa mtu yeyote (ambaye si serikali wala Serkali au taasisi ya serikali) kuhusiana na kitu chochote kilichofanywa au kutofanywa kabla ya siku ya utangazaji,

na iwapo sharti lolote limefanywa kinyume na kifungu kidogo hiki, sharti hilo litakuwa batili.

(3) Mamlaka ya kupanga siku ambayo Sheria Ndogo itaanza kutumika haitajumisha mamlaka ya kupanga siku tofauti kwa masharti tofauti ya Sheria hiyo, labda kama sharti la wazi limefanywa kwa ajili hiyo .

Kuwasilisha Kanuni Bungeni na kukataliwa

38.-(1) Kanuni au sheria ndogo zote zitawasilishwa Bungeni ndani ya kipindi cha siku sita za kukaa kwa Bunge kufuatia utangazaji utakaofuata wa kanuni katika Gazeti la Serikali.

(2) Bila ya kuathiri kifungu chochote kinachoelekeza vinginevyo katika sheria, iwapo Bunge litapitisha Azimio la kukataa kanuni yoyote ambayo taarifa ya azimio hilo litatolewa ndani ya siku 14 ya kukaa kwa bunge baada kanuni hizo zimekwishawasilishwa bungeni au kama kanuni zozote hazijawasilishwa Bungeni kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), kanuni hizo zitakoma kutumika , lakini bila ya kuathiri uhalali au kuhalalisha chochote kilichotendwa au kilichoachwa kutendwa katika wakati huo.

(3) Kifungu kidogo cha (2) kitatumika bila ya kujali kwambakipindi cha siku 14 kichotajwa katika kifungu kidogo hicho au sehemu ya kipindi hicho hakitatokea katika au wakati wa kikao hicho hicho cha Bunge kile ambacho kanuni zimewasilishwa Bungeni kinahusika .

(4) Bila ya kujali sharti lolote katika Sheria yoyote iliyo kinyume, kama Bunge katika kipindi chochote litapitisha azimio la kubadilisha kanuni yoyote au kuweka kanuni mbadala au sehemu ya kanuni ambayo imekataliwa na Bunge chini ya kifungu kidogo cha (2), katika kupitisha azimio lolote–

(a) linalorekebisha Kanuni au sehemu ya kanuni, kanuni iliyobadilishwa baada ya kuisha kwa siku saba, kutoka siku ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali ya taarifa iliyotolewa katika kifungu kidogo cha (5), itaanza kutumika kama ilivyorekebishwa.

(b) kuweka kanuni mbadala au sehemu ya kanuni, kanuni iliyobadilishwa baada ya kuisha kwa siku saba, kutoka siku ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali ya taarifa iliyotolewa katika kifungu kidogo cha (5), itaanza kutumika kama ilivyorekebishwa.

(5) Baada ya kupitishwa kwa Azimio kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha (4), Taarifa ya Azimio hilo itachapishwa kwenye Gazeti la Serikali ndani ya muda wa siku 21 baada ya kupitishwa kwa Azimio hilo.

(6) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 34, pale ambapo–

(a) kanuni hazikubaliki chini ya kifungu hiki; na

(b) kanuni hizo zilizorekebishwa au kufuta kanuni ambazo zilikuwa zinatumika mara kabla ya kanuni zilizotajwa kwa mara ya kwanza hazijaanza kutumika,

kukataliwa kwa kanuni hizo kutahuisha kanuni za awali kwenye ile siku na siku ya kukataliwa.

(7) Iwapo Sheria ambayo inatoa uwezo au inaelekeza kutengeneza kwa kanuni na mtu yeyote isipokuwa Rais,na inataka kanuni hizo kukubalika au kuthibitishwa na Rais au mtu mwingine yeyote au taasisi kabla kanuni hizo hazijatakuwa na nguvu za kisheria, kifungu kidogo cha (1) hakitatumika kwenye kanuni hizo isipokuwa kama zitakubalika au kuthibitiswa kama inavyotakiwa.

(8) Katika kifungu hiki, neno "kanuni" linajumuisha kanuni na Sheria Ndogo.

Tafsiri ya sheria ndogo

39.-(1) Maneno na misamiati inayotumiwa katika Sheria Ndogo itakuwa na maana sawa na Sheria iliyotungwa chini ya Sheria Ndogo.

(2) Rejeo katika Sheria Ndogo kwa neno "Sheria" litafafanuliwa kumaanisha rejeo kwenye Sheria ambayo, Sheria Ndogo imetungwa.

Kutajwa kwa sheria ndogo

40. Sheria Ndogo itatajwa kwa kurejea kwenye jina fupi kama litakuwepo, au kwa kurejea kwenye namba ya Tangazo inayotolewa kwenye Gazeti la Serikali.

Marejeo ya sheria kujumuisha sheria ndogo

41.-(1) Rejeo kwenye Sheria liltafchukuliwa kujumuisha rejeo kwenye Sheria Ndogo yeyote iliyotungwa kwa mujibu wa Sheria mama/kuu husika.

(2) Rejeo kwenye Sheria kwa Sheria ya mapokezi litafafanuliwa vilevile kuhusu rejeo kwenye Sheria Ndogo iliyotungwa chini ya Sheria mama.

Matendo chini ya sheria ndogo kuchukuliwa kama yamefanyika chini ya Sheria

42. Rejeo chini ya Sheria Ndogo kwenye sheria inayotumika litatafsiriwa kujumuisha rejeo kwenye Sheria Ndogo iliyotungwa chini ya Sheria mama.

Ada na tozo

43.-(1) Sheria Ndogo inaweza kuweka masharti ya kutozwa kwa ada na tozo zinazohusiana na jambo lolote kwa kutilia maanani masharti yaliyo wekwa katika Sheria Ndogo au katika Sheria ambayo, Sheria Ndogo imetungwa.

(2) Pale kifungu kimewekwa na Sheria Ndogo kinachohusu ada au tozo, Sheria Ndogo husika yaweza kuweka mojawapo au baadhi ya masharti yafuatayo–

(a) ada maalumu au tozo;

(b) kuweka kiwango cha juu au cha chini cha ada au tozo ya aina

nyingine;

(c) kiwango cha juu na cha chini cha ada au tozo;

(d) ada au tozo *kulingana na thamani ya kitu*;

(e) kulipwa kwa ada au tozo kwa pamoja au kwa chini ya masharti maalumu au mazingira yaliyoainishwa; na

(f) kupunguziwa, kusamehewa au kurejeshewa, kiasi chote au sehemu ya ada au tozo.

(3) Iwapo patakuwa na punguzo, msamaha au kurejeshewa, kwa ada yeyote au sehemu ya ada au tozo ilivyotozwa na Sheria Ndogo, punguzo hilo au msamaha au rejesho vyaweza kuchukuliwa kutumika au kutumika kwa ujumla au kwa masharti maalum–

(a) kuhusiana na mambo fulani au shughuli fulani au mambo au aina ya mambo au shughuli;

(b) kuhusiana na nyaraka fulani au aina ya nyaraka;

(c) pale tukio linapotokea au wakati tukio linapoacha kutokea;

(d) kuhusiana na watu wa aina fulani au tabaka la watu fulani; au

(e) kuhusiana na mchanganyiko wa mambo, shughuli, nyaraka, matukio au watu, na yaweza kuelezewa kutumika au kutumika kwa masharti yaliyoainishwa katika Sheria Ndogo au kwa uamuzi wa mtu yeyote aliyeainishwa katika Sheria Ndogo.

(4) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 2 cha kifungu hiki kitatumika kwenye Sheria Ndogo zilizotungwa chini ya mamlaka iliyopewa ya kutunga Sheria baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

SEHEMU YA SABA
UWEZO NA WAJIBU WA KISHERIA

Muda wa utekelezaji uwezo au wajibu kwa mujibu wa sheria

44. Pale ambapo Sheria imetoa mamlaka au kuweka wajibu, mamlaka hayo ya waweza kutekelezwa na wajibu huo kutekelezwa mara kwa mara wakati tukio litahitaji.

Rejeo kwa mshika ofisi itajumuisha warithi

45. Pale Sheria itatoa mamlaka au kutoa wajibu kwa afisa aliyeshika madaraka ya ofisi ya umma, mamlaka hayo yanaweza kutekelezwa na wajibu utafanywa na mtu ambaye kwa wakati uliopo atakuwa ameshika nafasi hiyo kihalali, anakaimu au kutekeleza majukumu ya ofisi.

Tafsiri ya maneno ya kuwezesha.

46.-(1) Pale ambapo sheria imetoa mamlaka kwa mtu kufanya au kupelekea kufanyika kwa kitu chochote au jambo, uwezo huo utachukuliwa kuwa umetolewa kwa watu, ili kumwezesha mhusika kufanya jambo au kusimamia kisheria utekelezwaji wa kitu au jambo.

(2) Bila ya kuathiri ujumla wa matakwa ya kifungu kidogo cha

(1), pale sheria inatoa uwezo–

(a) wa kutoa ,kuzuia ,kudhibiti au kusimamia jambo lolote, uwezo huo utajumuisha uwezo wa kufanya hivyo sawa kwa kutoa leseni au kusajili au kutoa vibali na uwezo wa kuzuia vitendo kwa njia ya makatazo, kudhibiti au kusimamia kitu hicho kunaweza kuepukwa;

(b) kutoa leseni, kusajili,kupangisha, kutoa hakimiliki, kibali,mamlaka, kuithibitisha au kutoa msamaha, uwezo huo unajumuisha uwezo wa kutoa masharti kulingana na, leseni, usajili,kupangisha, kumiliki, kibali,mamlaka, idhini au msamaha vinaweza kutolewa;

(c) kuithibitisha mtu yoyote, jambo au kitu, na uwezo huo utajumuisha uwezo wa kufuta idhini iliyotolewa;

(d) kutoa maelekezo, na uwezo huo utajumuisha uwezo wa kutoa maelekezo sawa kwa aina ya makatazo.

(3) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (4) cha kifungu cha 2, kifungu hiki kitatumika kwenye Sheria zilizotungwa au kupitishwa baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Uwezo wa kutoa leseni, nk., kwa kwa hiari

47.-(1) Pale ambapo sheria inapotoa uwezo kwa mtu kutoa leseni au kuhuisha,kutoa au kuisajiri tena leseni yeyote, kusajili,kupangisha, kutoa hakimiliki,mamlaka, kuthibitisha, kutoa kibali, au msamaha, mtu huyo aliyepewa uwezo huo anaweza kutumia mamlaka yake ,kutoa, kuhisha leseni,au kukataa kutoa, usajili tena leseni hiyo,kusajiri,kupangisha, kumiliki, mamlaka, kuidhinisha, kumpakibali au kusamehe.

(2) Hakuna katika Kifungu hiki kitakachoathiri haki iliyotolewa na sheria nyingine yeyote kwa mtu yeyote kukata rufaa dhidi ya kukataa kutoa,kumpa, kuhuishiwa leseni yeyote, kusajiliwa,kupangisha, kumiliki, kuidhinishiwa au kupewa msamaha.

Uwezo wa kuteua unajumuisha uwezo wa kusimamisha, au kuondoa madarakani nk.

48.-(1) Pale ambapo Sheria inapotoa mamlaka au inapotoa wajibu kwa mtu yeyote kuteua afisa au nafasi,ikijumuisha uteuzi wa kukaimu nafasi, mtu aliyepewa mamlaka hayo atakuwa pia na uwezo wa–

(a) kumuondoa, kumsimamisha mtu aliyeteuliwa kwenye ofisi au nafasi hiyo, na kumteua tena au kumrejesha kwenye nafasi hiyo,mtu yeyote aliyeteuliwa kutekeleza uwezo au wajibu huo;

(b) pale mtu aliyeteuliwa kushika madaraka ya ofisi au nafasi, atasimamishwa au atashindwa, au anaelekea kushindwa kwa sababu yoyote kutekeleza kazi za ofisi hiyo au nafasi aliyoteuliwa, atateua mtu mwingine kukaimu nafasi hiyo kwa muda kwa niaba ya yule aliyeteuliwa, aliyesimamishwa kwa muda wote ambao mtu huyo amesimamishwa au hawezi kutekeleza wajibu wake, lakini mtu huyo atateuliwa kukaimu

kama tu anastahili nakuwa na sifa za kuteuliwa kwenye ofisi au nafasi hiyo; na

(c) kuainisha muda ambao mtu yeyote aliyeteuliwa kutekeleza mamlaka au wajibu atashika madaraka ya nafasi aliyoteuliwa.

(2) Kwa mujibu wa aya ya (b) ya kifungu kidogo cha (1) "sababu" linajumuisha–

(a) ugonjwa;

(b) kutokuwepo kwa muda, ndani ya Jamhuri ya Muungano; na

(c) mgongano wa kimaslahi.

(3) Uhalali wa jambo lolote lililotendwa au kufanywa na mtu yeyote kwa madai ya kuteuliwa chini ya ibara ya (c) ya kifungu kidogo cha (1) haitahojiwa kwa madai kuwa uteuzi wake haukukamilika au ulikoma.

(4) Pale ambapo Sheria imetoa mamlaka au imetoa wajibu kwa mtu yoyote kufanya uteuzi kwenye ofisi au nafasi na uwezo huo au wajibu huo waweza kutekelezwa tu baada ya uteuzi au mapendekezo ya majina, au kama uteuzi huo shurti uridhiwe, au uthibitishwe au ukubaliwe na watu wengine, basi uwezo uliotolewa kwa mujibu wa aya ya (a) hadi (c) za kifungu kidogo cha (1) utatumiwa kwa kuzingatia uteuzi au mapendekezo au kwa kuzingatia uthibitisho, kuungwa mkono au ridhaa.

(5) Hakuna jambo lolote katika kifungu hiki litaathiri muda wa kushika madaraka ya ofisi au wadhifa wa mtu yoyote, kwa mujibu wa masharti ya Sheria yeyote ya Bunge.

Uteuzi kwa jina au ofisi, nk. Na uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi,

49.-(1) Pale ambapo Sheria inatoa mamlaka au kutoa wajibu kwa mtu kuteua au kutaja mtu na kumpa madaraka ya–

(a) kufanya kazi yeyote;

(b) kuwa mjumbe wa Bodi, baraza la nyumba, kamisheni, kamati au baraza au kitu kingine kilichoundwa kwa namna hiyo; au

(c) kuwa au kufanya jambo lolote,

mtu huyo aweza kuteua kwa kumtaja mtu kwa jina lake au kwa kuteua mtu aliyeshika kwa masharti ya uteuzi wa ofisi yake; na uteuzi wowote wa afisa anayeshikilia ofisi hiyo kutatafsiriwa kama uteuzi wa mtu huyo mara kwa mara atakayeshikilia nafasi hiyo,tatakayekaimu, au atakayekuwa akitekeleza kihalali kazi za ofisi hiyo.

(2) Pale kwa au chini ya Sheria yoyote imetoa mamlaka kwa mtu yoyote au mamlaka kuteua wajumbe wa bodi, kamisheni, kamati au chombo chochote kinachofanana nayo, mtu huyo au, mamlaka hiyo,inaweza isipokuwa kama itaenda kinyume na dhamira itakayojitokeza itateua au kuweka kanuni, za uteuzi wa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti na katibu wa bodi, kamisheni, kamati au chombo kingine kinachofanana na aina hiyo.

Uwezo wa walio wengi, akidi nk.

50.-(1) Pale ambapo Sheria inapotoa mamlaka au majukumu kwa

bodi au idadi ya watu ambao hawapungui watatu,kazi hiyo inaweza ikafanywa na wengi kati ya watu hao.

(2) Pale ambapo Sheria imeunda bodi, kamisheni, kamati au baraza au aina yeyote ya chombo kinachofanana na hivyo na yenye wajumbe 3 au zaidi (katika kifungu hiki ikijulikana kama "ushirika")–

(a) katika mkutano wa jumuiya, idadi ya wajumbe iko sawa na–

(i) angalau nusu ya idadi ya wajumbe iliyotolewa na sheria yeyote ya bunge, kama namba hiyo imetajwa maalum;na

(ii) kama namba ya wajumbe imeainishwa katika sheria haikutaja idadi kamili, lakini ipo katika kiwango cha juu au chini, angalau nusu ya idadi ni wanachama wapo katika ofisi kama idadi hiyo iko katika kiwango, kinachofikia akidi; na

(b) tendo au jambo lolote liliofanywa na idadi kubwa ya wajumbe waliohudhuria kwenye mkutano, kama wajumbe waliopo wanafikia akidi, kuchukuliwa kuwa imeamuliwa na ushirika.

Utekelezaji wa uwezo unaweza kusahihishwa

51. Pale ambapo Sheria inatoa uwezo au jukumu kwa mtu kufanya jambo au kitu cha kiutawala au cha madaraka au kufanya uteuzi wowote, uwezo au jukumu linaweza kufanywa au kutekelezwa mara kwa mara kama itakavyoonekana inafaa, kusahihisha makosa yoyote au kuacha jambo ambalo lilitakiwa kufanywa huko nyuma au kutekelezwaji wa uwezo au jukumu, bila ya kujali kuwa uwezo au jukumu hilo haliwezi kutekelezeka kwa ujumla au kufanyika mara kwa mara.

Athari ya uteuzi wakati afisa anayestaafu yuko likizo

52. Wakati afisa anayeshikilia madaraka katika ofisi yeyote iliyoundwa chini ya Sheria yeyote yuko kwenye likizo akisubiri kuachia madaraka kwenye ofisi yake, itakuwa halali kisheria kwa mtu mwingine kuteuliwa rasmi kushika wadhifa wa ofisi hiyo.

"Inaweza au anaweza" ina maana ya hiari na neno "ata" au "ita" lina maana ya lazima

53.-(1)Pale katika Sheria, litumikapo neno "inaweza" au "anaweza" litatumika kutoa uwezo, neno hilo litatafiriwa kumaanisha kuwa uwezo uliotolewa unaweza kutekelezeka au kutokutekelezeka kwa kuamuwa.

(2) Katika Sheria litumikapo neno "ata" au "ita" litatumika kutwisha jukumu, na neno hilo litatafsiriwa kumaanisha majukumu yaliotwishwa sharti yafanyike.

Uwezo wa bodi n.k havitaathiriwa kwa nafasi iliyowazi au mapungufu mengine

54. Pale ambapo bodi, baraza la nyumba, tume, kamati au baraza au chombo kingine kinachofanana na hicho ,yaweza ikawa shirika au kampuni ,litaanzishwa chini ya Sheria, mamlaka ya chombo hicho havitaathiriwa na–

(a) kuwepo kwa nafasi yoyote ya wazi ya mwanachama wa

bodi;

(b) mapungufu yoyote yatakayojitokeza katika uteuzi au sifa ya mtu yeyote aliyetarajiwa kuwa mjumbe wa bodi au kukaimu nafasi ya mjumbe;

(c) kasoro ndogo itakayotokea katika kuitisha au kuendesha mikutano ya bodi, au

(d) kuwepo au kushiriki katika mikutano kwa mtu ambaye hastahili kuwepo au kushiriki katika mkutano.

Utekelezaji wa mamlaka Fulani kwa anayekasimu

55. Pale ambapo Sheria ianelekeza kuwa utendaji wa kazi yoyote na mtu utategemea na maoni, imani au ufahamu wa mtu huyo juu ya kitu chochote na kazi hiyo alivyokasimiwa chini ya sheria yoyote, kazi hiyo inaweza kutekelezwa na muwakilishi kwa kuzingatia maoni, imani, au ufahamu wa mtu anayekasimu kuhusiana na jambo hilo.

Rejeo kwenye eneo kwa kutumia mipaka

56.-(1) Pale Sheria inaporejea au kutaja sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano kwa tamko maalum, itatumika kumaanisha, kwa jinsi hiyo, sehemu hiyo kama itakavyotajwa ambayo mara kwa mara imefafanuliwa, mpaka wake umewekwa au kuainishwa, isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo.

(2) Pale ambapo eneo limetengwa kwa, kurejea kwenye eneo lolote ambalo limebadilishwa, marejeo katika sheria yeyote juu ya eneo liliyobadilishwa kutoka kwenye eneo la zamani, yatafafanuliwa kama rejeo la eneo lililotengwa.

Tafsiri ya Uwezo wa kukasimu

57.-(1) Pale Sheria inatoa uwezo kwa mtu kukasimu utekelezaji wowote wa mamlaka au majukumu ya wajibu wowote aliopewa au kuwekwa juu yake chini ya sheria–

(a) uwakilishi huo hautamzuia mtu aliyekasimiwa, kutekeleza na kufanya katika muda wowote mamlaka au majukumu yake aliyokasimiwa;

(b) uwakilishi huo unawaweza kufanywa kwa kuzingatia masharti yoyote, sifa, ukomo au vigezo maalumu ambavyo mtu aliyeteuliwa anaweza kuainisha;

(c) iwapo uwakilishi unaweza kufanywa tu kwakuthibitiswa na uteuzi huo na marekebisho yoyote ya kukasimu, yanaweza yakafanywa kwa kuzingatia masharti,sifa , ukomo au sababu maalumu ambazo mtu aliyethibitishwa ataziainisha;

(d) uwakilishi huo unaweza ukafanywa kwa mtu aliyeainishwa au watu lililoainishwa katika daraja, au yaweza ikafanywa kwa mtu aliyeshikilia madaraka au watu walioshikilia madaraka kwa wakati huo wanakuwa kwenye ofisi au aina za ofisi;

(e) uwakilishi huo unaweza kurekebishwa au kufutwa kwa hati iliyoandikwa na kusainiwa na mtu aliyekasimiwa madaraka;

(f) ikiwa mamlaka aliyopewa mtu kwa ambapo uwezo wa kuteua mwakilishi umetolewa kwa mtu kwa kuzingatia masharti yaliyoanzisha ofisi, kukasimu huko hakutachukuliwa kuwa na madhara kwa sababu tu za kubadilishwa, mtu anayeshikilia ofisi kihalali, anayekaimu au kutekeleza kazi za ofisi hiyo.

(2) Kukasimu madaraka kutachukuliwa kujumuisha uwakilishi unaoambatana au uanohusiana na majukumu, na kukasimu kwa uwakilishi huoutachukuliwa kujumuisha uwakilishi unaoambatana au kuhusiana na uwezo huo.

(3) Pale chini ya Sheria, kitendo au jambo laweza au linatakiwa kufanywa kwa kurejea kwenye au kuhusiana na mtu, na mtu huyo kwa mujibu wa sheria amepewa uwezo wa kukasimu kazi iliyopewa au kuwekwa kwake kuhusiana na au matokeo yanayotokana na kufanya kwa kitendo hicho au jambo hilo, kwa kurejea kwenye kitendo au kuhusiana na mtu ambaye amekasimiwa jukumu hilo.

Ni nani ataweka lakiri ya kampuni au shirika

58. Pale ambapo Sheria inaruhusu bodi au kamati kufanya kitu chochote, jambo lolote, au kitu itachukuliwa kumaanisha kwambakitendo hiko,jambo hilo au kitu hicho kinaweza au kufanywa na bodi au kamati kama itatokea.

Haki za Serikali

59. Hakuna Sheria kwa namna yoyote itakayoibana au kuathiri haki za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa kama Sheria hiyo imetamka, au kama itaonekana ni muhimu kwamba Serikali ya Jamhuri kubanwa na sheria hiyo.

SEHEMU YA NANE
MASHARTI KUHUSU, MUDA NA UMBALI

Kukokotoa Muda

60.-(1) Katika kukokotoa wakati kwa mujibu wa Sheria ya Bunge–

(a) pale ambapo muda umeelezwa kwa, juu ya au katika siku iliyoainishwa, siku hiyo itajumuishwa katika kipindi hicho;

(b) pale kipindi kimeelezwa kuwa kinakokotolewa tokea, au baada , siku maalumu, siku hiyo haitajumuishwa katika kipindi hicho;

(c) pale ambapo jambo fulani linatakiwa kufanywa ndani ya muda kabla ya siku iliyoainishwa, muda huo hautajumuisha kwenye siku iliyotajwa;

(d) pale ambapo muda umeelezwa kukoma mnamo,juu au ndani ya siku iliyotajwa, au kuendelea hadi siku iliyotajwa, siku hiyo itajumuishwa katika kipindi hicho;

(e) pale ambapo muda wa kutendwa jambo fulani unakoma,

au unaangukia katika siku ambayo imetolewa katika orodha, jambo hilo laweza kufanywa katika siku inayofuata ambayo haijaondolewa katika orodha;

(f) pale ambapo kuna rejeo ya idadi ya siku kamili, au "angalau" au "isiyopungua"au "isiyozidi", idadi ya siku yaliyotajwa, siku hizo zitahesabiwa kwa kuondoa siku ambazo zimo ndani ya matukio yaliyotajwa;

(g) pale ambapo kuna rejeo kwenye idadi ya siku ambazo hazikutajwa au "angalau siku", au "isiyopungua siku" idadi ya siku katika matukio mawili, katika kuhesabu idadi ya siku inatakiwa kuondoa siku ambayo tukio la kwanza linatokea na kuondoa siku ambapo tukio la pili linatokea zitaondolewa katika orodha;

(h) Pale ambapo kitendo au mwenendo umeelekezwa moja kwa moja au unaruhusu kufanyika au kufanywa katika siku fulani, au kwenye hiyo siku au kabla ya siku fulani, basi kama siku hiyo imeondolewa katika orodha, tendo hilo au mwenendo huo vitafanywa au vitahesabika kuwa vimefanywa katika siku muafaka iwapo vitafanyika aukuchukuliwa kufanyika siku ya pili ambayo sio siku ambayo imeondolewa kwenye orodha.

(2) Kwa minajili ya kifungu hiki, "siku zilizoachwa nje ya orodha" ina maana siku za Jumamosi, Jumapili au siku yoyote ya likizo au ile sehemu inayohusiana na siku ambayo tukio, tendo, kitu, hatua au mwenendo kuchukuliwa.

Kuhesabu miezi

61.-(1) Katika Sheria, neno "mwezi" lina maana ya mwezi wa kalenda, ikimaanisha, mwezi unaohesabiwa kwa kufuata kalenda.

(2) Kama kipindi cha mwezi mmoja kilichoainishwa katika Sheria ya Bunge kinaanza katika siku isiyokuwa siku ya kwanza kati ya miezi 12 ya kalenda, siku hiyo itahesabiwa kuanzia siku ambapo inaanza hadi siku kama hiyo ya mwezi unaofuata, baada ya kutoa moja, au kama hakuna tarehe iliyo sawa, itakuwa siku ya mwisho ya mwezi huo.

Kwa mfano: mwezi unaoanzia tarehe 15 Januari utashia tarehe 14 Februari na mwezi unaoanzia tarehe 30, 31 Januari utaishia tarehe 28 Februari (au 29 Februari katika mwaka mrefu).

(3) Kama kipindi kilichotajwa katika Sheria ya Bunge ni miezi 2, 3 au mwezi mrefu, kitaanza kuhesabiwa kuanzia tarehe kipindi hicho kinatakiwa kuanza hadi namba inayowiana, ukiondoa moja ,katika ya pili, ya tatu au miezi mingine inayofuata baada ya hapo, au kama hakuna tarehe zinazofanana, siku ya mwisho ya mwezi huo unaofuata.

Kwa mfano: kipindi cha miezi 6 kinachoanza tarehe 15 Agosti, kinaishia tarehe 14 Februari na kipindi cha miezi 6 kinachoanzia tarehe 30 au 31 Agosti kinaishia tarehe 28 Februari (au tarehe 29 Februari katika mwaka mrefu).

Masharti palemuda haujapangwa

62. Pale ambapo muda kamili haukutajwa au kuruhusu kufanya tendo au kitu, kitendo hicho au jambo hilo laweza kufanywa kwa haraka iwezekanavyo, na kwa nyakati mbalimbali, kadri matukio yatakavyo jitokeza.

Tafsiri uwezo kuongeza muda

63.-(1) Pale ambapo Sheria ya Bunge imeweka muda maalumu au imeruhusu jambo fulani kutendwa au kufanya mwenendo wowote na kimahakama imepewa uwezo au mamalaka nyingine kuongeza muda, uwezo huo waweza kufanywa na mahakama au mamlaka nyingine ingawaje kuongeza muda hakukufanywa mpaka baada ya kuisha kwa muda uliowekwa au kuruhusiwa.

(2) Kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) kifungu hiki yatumika kuhusiana na Sheria za Bunge ziliotungwa au kupitishwa baada ya kuanza kutumika kwa Sheria hii.

Mkengeuko wa matumizi ya fomu, taratibu

64. Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo, fomu zilizoainishwa, kukengeuka huko hakutaathiri msingi na hakutahesabiwa kupotosha, kupunguza nguvu au uzito wa taarifa zake.

Vipimo vya umbali

65. Katika kupima umbali kwa ajili ya madhumuni ya Sheria yeyote ya Bunge, umbali utapimwa kwa mstari ulionyooka katika mlalo ulio sawa.

SEHEMU YA TISA
TARATIBU NA ADHABU

Mashauri ya wadhifa wa kiofisi hayakomi baada ya kifo.

66. Mashauri ya madai au jinai dhidi ya mtu yeyote kwa misingi ya wadhfa wake hayatasimamishwa au kukoma kutokana na kifo, kujiuzulu, kutokuwepo au kuondolewa madarakani kwa mtu huyo, bali yaweza kuendelezwa na au dhidi ya mtu mwingine yeyote,kama itakavyowezekana, na mtu ambaye, atakuwa ameshikilia madaraka ya ofisi hiyo.

Kanuni za mahakama

67.-(1) Katika Sheria ya Bunge, maneno “kanuni za mahakama” kuhusiana na mahakama, yana maana ya kanuni zilizotungwa na mamlaka yenye uwezo kwa wakati uliopo, wa kutunga kanuni au amri za kusimamia utendaji na mwenendo katika mahakama husika.

(2) Uwezo wa mamlaka uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) unajumuisha uwezo wa kutunga kanuni za mahakama kwa ajili ya sheria yoyote inayoelekeza au kuruhusu jambo lolote lifanywe na au kwa mujibu wa kanuni za mahakama.

kutolewa kwa adhabu si kizuizi cha kesi ya madai

68. Kutolewa kwa adhabu au faini na au kwa mujibu wa mamlaka ya Sheria yeyote, kama hakuna masharti yaelekezavyo vinginevyo, hakutatoa ahueni ya wajibu kwa mtu kushtakiwa kwa

madhumuni ya kumwajibisha mtu huyo kutoa fidia kwa mtu yeyote aliyejeruiwa

Upatikanaji wa faini na adhabu

Sura ya .20

69. Pale ambapo faini au adhabu za aina nyingine zimetozwa chini ya Sheria, na hakuna taratibu zilizowekwa na Sheria za namna ya upatikanaji wa faini au adhabu, itachukuliwa kwamba faini au adhabu hizo zinaweza kutozwa au kupatikana kwa dharura, chini ya vifungu vya Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai kwa mashauri ya dharura kwa njia ya muhtasari au chini ya sheria nyingine yoyote ambayo itakuwa inatumika kwa ajili hiyo.

Kutia hatiani mara dufu

70. Pale ambapo tendo limetamka kosa mara mbili au zaidi iwe ni kwa mujibu wa Sheria moja au vinginevyo, mkosaji atashtakiwa kwa kosa lolote au makosa yote lakini hataadhibiwa mara mbili kwa kosa la aina moja.

Matumizi ya Sheria ya Kanuni za Adhabu kwa Makampuni.

71.-(1) Sheria yoyote inayo ainisha makosa ambayo adhabu zake baada ya kutiwa hatiani, au kwa kutiwa hatiani kwa muhtasari, itahusisha pia kampuni, mashirika, taasisi na watu binafsi.

(2) Pale ambapo Sheria kukamatwa kwa mali kwa ajili ya kufidia mwathirika wa kosa,au adhabu inatolewa kwa kwa mtu aliyeudhiwa, faini, tozo au fidia hiyo italipwa kwa shirika, kampuni au taasisi iliyodhurika kama taasisi hiyo itakuwa ni sehemu ya waasirika wa kosa husika.

(3) Isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo, pale ambapo adhabu imeainishwa katika Sheria dhidi ya kosa ambalo adhabu yake haijumuishi kulipwa kwa faini, mahakama ambayo inasikiliza kesi hiyo inaweza , kwa mkosaji ambaye ni shirika, kampuni au taasisi kutoza faini–

(a) pale ambapo adhabu ni kifungo kisichozidi miezi sita, faini itozwe ya Shilingi Milioni Mbili;

(b) pale ambapo adhabu ni kifungo kisichozidi miezi sita lakini kisochozidi mwaka mmoja itatolewa, faini itozwe ya Shilingi Milioni Tatu;

(c) pale ambapo adhabu ni kifungo kinachozidi mwaka mmoja lakini hakizidi miaka miwili itatolewa, itozwe faini ya Shilingi Milioni Tano;

(d) pale ambapo adhabu ni kifungo kinachozidi miaka mitatu itatolewa, itozwe faini ya Shilingi Milioni Kumi.

Masharti ya makosa chini ya sheria mbili au zaidi

72. Pale ambapo tendo la aina moja limeainishwa kama kosa chini ya Sheria mbili au zaidi, mkosaji isipokuwa kama dhamira itajitokeza, litashitakiwa na kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria yoyote mojawapo, lakini hataadhibiwa zaidi ya mara moja kwa kosa linalofanana.

Marekebisho ya adhabu

73. Pale ambapo tendo limepelekea kosa,na adhabu kwa kosa hilo imerekebishwa kati ya muda ambao kosa hilo limetendeka na baada ya kutiwa hatiani, mshtakiwa isipokuwa kama marekebisho ya adhabu yameelekeza dhamira yake vinginevyo,, ataadhibiwa kwa kutumia adhabu iliyokuwa ikitumika wakati wa kutendeka kwa kosa hilo.

Maagizo ya adhabu ya juu , ya chini, ya kila siku na ya pamoja

74.-(1) Pale ambapo Sheria ya Bunge imeainisha adhabu kwa kosa, ile adhabu iliyoainishwa ndiyo itakayokuwa ya juu kwa kosa hilo.

(2) Pale ambapo Sheria imeainisha adhabu zaidi ya moja kwa kosa moja, matumizi ya neno "na" katikati ya adhabu hizo mbili, itamaanisha adhabu hizo zaweza kutozwa moja pekee au zitozwe zote mbili kwa pamoja.

(3) Pale ambapo Sheria imeainisha kiwango cha juu cha adhabu na cha adhabu ya chini kwa kosa moja, kosa hilo laweza kutolewa adhabu isiyopungua kiwango cha chini cha adhabu na isiyozidi kiwango cha juu.

(4) Pale ambapo Sheria imeainisha kiwango cha chini cha adhabu kwa kosa, kosa hilo litatolewa adhabu isiyo chini ya kiwango cha chini cha adhabu.

(5) Pale ambapo Sheria imeainisha adhabu inayotolewa au kutozwa kila siku kwa kosa llilotamkwa, elekezo hilo lina maana kwamba, adhabu isiyopungua adhabu iliyotamkwa kwa kila sikuinaweza, ikatolewa na nyongeza ya adhabu nyingine kwa kosa hilo, na itatozwa kwa kila siku au sehemu ya siku ambapo kosa hilo litaendelea kutendwa.

Vifungu vinavyohusu kujaribu

75. Kifungu katika Sheria kinachopelekea kosa, isipokuwa kama dhamira itajitokeza litachukuliwa kama jaribio la kutaka kutenda kosa litakuwa ni kosa chini ya kifungu hicho, linalostahili adhabu kana kwamba kosa lenyewe limetendwa.

Utoaji wa mali au vitu vilivyotwaliwa

76.-(1) Pale ambapo chini ya Sheria yoyote inaelekeza kukamatwa kwa mnyama au kitu chochote kwa amri ya mahakama au mamlaka yoyote, itaweza isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo au kama itaelezwa na sheria kuchukuliwa na mtu yeyote ,kuchukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, na mapato yote yatakayopatikana, kama yataamuliwa na mamlaka husika kuuzwa, gharama zitalipwa na kuhesabiwa kama sehemu ya mapato ya umma, isipokuwa kama vifungu vingine vitaelekeza vinginevyo.

(2) Hakuna kitu chochote katika kifungu hiki kitakachoathiri kifungu chochote katika Sheria yoyote ya Bunge ambayo kwayo, sehemu ya faini au mali iliyotwaliwa, au mwenendo wa mali yoyote iliyotwaliwa, vimeelekezwa vitwaliwe na mtu yeyote au vitolewe na mtu au mamlaka yoyote kwa mtu yeyote .

Uwajibikaji wa mwajiri au mkuu

77. Pale kosa lolote chini ya Sheria limetendwa na mtu kama

wakala au mtumishi , isipokuwa kama dhamira nyingine imeelezwa, na wakala huyo au mwajiriwa, pamoja na mwajiri au mkuu wa sehemu hiyo watakuwa wametenda kosa na endapo watapatikana na hatia wanaweza kushtakiwa na kuadhibiwa sawia, isipokuwa kama ataithibitishia mahakama kwamba hakujua chochote kuhusu uhalifu huo, na kwa kutumia busara ya kawaida, asingeweza kufahamu kutendeka kwa kosa hilo.

Ushahidi wa agizo , kibali au ridhaa ya mtumishi wa umma

78. Wakati wowote ambapo amri au agizo la kiutawala, idhini au kibali cha afisa wa serikali kinahitajiwa kabla ya kuanza kuendesha kesi au mashauri, hati yoyote inayoonyesha kuwa amri, agizo au ridhaa imetolewa, itachukuliwa kama ushahidi wa kutosha katika kesi au mashauri, bila ya kuhitaji ushahidi mwingine kuthibitisha kwamba saini iliyoko kwenye hati hiyo, ni ya afisa wa serikali mhusika.

Utekelezaji wa mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) wakati hayupo

79. Mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka yanaweza kutekelezwa na Afisa wa Sheria aliyeteuliwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa madhumuni hayo, iwapo Mkurugenzi wa Mashtaka. atakuwa hayupo Makao Makuu ya Ofisi yake, au atakuwa hawezi kutekeleza majukumu yake kutokana na ugonjwa au kwa sababu nyingine yoyote ,

Tamko la adhabu mwishoni mwa kifungu

80.-(1) Pale ambapo katika Sheria, adhabu–

(a) imeainishwa bila ya masharti yoyote kutajwa mwishoni mwa kifungu,

(b) imeainishwa mwishoni mwa kifungu kidogo cha Sheria, lakini sio chini ya kifungu;au

(c) imeainishwa mwishoni mwa kifungu cha Sheria na kuelezwa kuwa kitatumika kwenye na kifungu kidogo katika kifungu hicho,

basi, isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo, kuainishwa huko kunamaanisha kwamba ukiukwaji wa kifungu au kifungu kidogo, au kama itakavyohusu, kifungu chochote kidogo, ni kosa ambalo linaadhibiwa kwa adhabu isiyopungua ile iliyotajwa.

Makosa yanayoendelea

81.-(1) Pale ambapo–

(a) kwa mujibu au chini ya Sheria, kitendo au kitu inatakiwa au imeelekezwa kifanywe ndani ya muda fulani au kabla ya wakati fulani; na

(b) kushindwa kutenda kitendo hicho au kitu hicho ndani ya muda au kabla ya wakati ilioelezwa katika aya(a) litakuwa ni kosa; na

(c) kitendo hicho au jambo hilo litafanyika ndani ya muda uliotajwa au katika wakati uliotajwa kama ilivyoelezwa aya (a), vifungu vifuatavyo vitahusika–

(i) jukumu la kutenda kitendo au jambo hilo litaendelea, bila ya kujali kwamba kipindi

kilichopangwa kimepita au muda uliowekwa umepita, hadi hapo kitendo hicho au jambo hilo litakuwa limetendwa;

(ii) pale ambapo mtu ametiwa hatiani kwa kosa ambalo, kwa mujibu aya (i) limetokana na kushindwa kutenda kitendo au jambo baada ya kuisha kwa kipindi kilichowekwa au baada ya muda uliopangwa,kama utakuwepo , mtu huyo atakuwa ametenda makosa tofauti, na kosa jingine yanayofuata kwa kila siku baada ya siku ya kuhukumiwa, kwa kosa hilo au jambo hilo kwa kila siku inayoendelea; na

(iii) isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo, adhabu itozwayo kwa kila kosa pekee na makosa mengine yanayofuata itakuwa ni kiasi kilicho sawa na Shilingi Elfu Thelathini.

(2) Pale ambapo–

(a) kwa mujibu wa au chini ya Sheria, tendo au kitu kinatakiwa au kimeelekezwa kifanywe lakini hakuna kipindi au muda uliowekwa wa kufanya kitendo au kitu hicho; na

(b) kushindwa kufanya kitendo hicho au kitu hicho ni kosa; na

(c) mtu anatiwa hatiani kwa kosa la kushindwa kufanya kitendo hicho au kufanya jambo hilo,

mtu huyo atakuwa ametenda kosa la kipekee na kosa jingine linalofuata kwa kila siku baada ya siku ya kutiwa hatiani,na iwapo atashindwa kutenda kitendo hicho au kufanya jambo hilo kunaendelea na, isipokuwa kama imeelekezwa vinginevyo, adhabu itozwayo kwa kila kosa ambalo ni tofauti na makosa mengine yanayofuata atatozwa kiasi cha Shilingi Elfu Thelathini.

(3) Mashtaka dhidi ya mtu mmoja kwa makosa mbalimbali chini ya aya ya (ii) cha kifungu kidogo cha (1) au kifungu kidogo cha (2) yaweza kuunganishwa katika taarifa moja au mashtaka kama makosa husika yanahusiana na kushindwa kufanya kitendo kinachofanana au kitu.

(4) Kama mtu atatiwa hatiani kwa kosa zaidi ya mojawapo ya chini ya aya (ii) cha kifungu cha (1) au zaidi ya makosa chini ya kifungu kidogo cha (2), mahakama yaweza kutoa adhabu moja kwa makosa yote ambayo mtuhumiwa ametiwa hatiani chini ya kifungu kidogo husika, lakini adhabu yake haitazidi kiwango cha juu cha adhabu inayoweza kutozwa kama adhabu hiyo ingetozwa otfauti kwa kila kosa.

SEHEMU YA KUMI
MASHARTI YA JUMLA

Uwasilishaji wa Nyaraka kwa njia

82.-(1) Pale ambapo Sheria ya Bunge inaruhusu au kutaka kuwa

ya posta

hati iwasilishwe kwa njia ya posta, iwapo neno "wasilisha" au maneno mengine kama vile, "patia", "kupata", au "peleka" au maneno mengine ya yanayofanana, au tafsiri itakayotumika ,kuwasilisha kutachukuliwa kuwa kuwasilisha kwa utimilifu kwa kuandika anuani sahihi na kuposti kwa (kulipa gharama stahiki) hati ya kupeleka barua kwa kutumia anuani ya mwisho ya anayepelekewa, na isipokuwa kama itathibitiswa vinginevyo, itahesabiwa kwamba kutaathiri muda ambao barua hiyo ingewasilishwa kwa njia ya kawaida ya posta.

(2) Pale ambapo Sheria inaruhusu au inaelekeza kuwa hati ya kuwasilishwa iwasilishwe kwa njia ya rejesta ya posta, hata kama neno la "wasilisha" au maneno mengine kama "patia", "peleka" au "wasilisha" au maneno mengine ya msemo kama huo yametumika, basi kama hati hiyo inasomeka na inakubalika kwa kuwasilishwa kama barua iliyothibitishwa, kuwasilishwa kwa hati hiyo kwaweza kufanywa ama kwa rejesta ya posta, au kwa njia ya barua iliyothibitishwa.

(3) Vifungu vidogo vya (1) na (2) vitahusika, isipokuwa kama dhamira nyingine inaonekana na kifungu kidogo cha (2) hakitahusika pale ambapo Sheria imeelekeza kutolewa kwa uthibitisho au stakabadhi iliyosainiwa na mtu ambaye hati hiyo imepelekwa kupitia anuani yake na hiyo itaashiria kuwa hati hiyo imewasilishwa kwa mhusika.

Uwasilishaji wa Nyaraka kwa ujumla

83. Pale ambapo Sheria inaruhusu au kuelekeza kuwa hati iwasilishwe, hata kama neno "wasilisha", "patia","peleka" au "wasilisha" au neno lingine kama hilo au msemo wa aina hiyo umetumika lakini bila ya kuelekeza kuwa uwasilishwaji ufanywe kwa namna gani, basi hati hiyo itakuwa imewasilishwa kikamilifu kwa mhusika:–

(a) kwa kupeleka hati hiyo kwa mtu huyo binafsi; au

(b) kwa njia ya posta kulingana na maelekezo ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 82; au

(c) kwa kuacha hati kwa mhusika kwenye makazi yake ya kawaida au yale ya mwisho yaliyokuwa yanafahamika, au kama ni mkuu wa biashara makao makuu ya biashara zake, au

(d) kama mhusika ni kampuni au shirika au taasisi au chama, au jumuiya ya watu (bila ya kujali kama imeandikishwa kama kampuniau la), kwa kuwasilisha, au kuiacha nyaraka au kuiposti kama barua kwa anuani ya kampuni, shirika, taasisi au chama kwenye makao makuu ya biashara au ofisi kuu zilizomo ndani ya Jamhuri ya Muungano.

Lugha ya sheria za Tanzania

84.-(1) Lugha za Sheria za Tanzania zitakuwa ni Kiswahi au Kiingereza au lugha zote mbili.

(2) Pale ambapo Sheria yoyote imetafsiriwa kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine na kuchapishwa kwa lugha zote mbili, na iwapo itatokea mgongano au kutakuwa na mashaka ya maana ya maneno au maelezo, lugha ambayo imetumika wakati wa kupitisha Sheria hiyo na

Bunge, ndiyo itakayokuwa ya kipaumbele

(3) Pale ambapo Sheria imeandikwa kwa lugha zote mbili na ukatokea mgongano au mashaka kuhusiana na maana ya neno lolote au maelezo, tafsiri ya Kiingereza ndiyo itakayotumika.

Kufutwa kwa Sheria ya Bunge Na 30 ya mwaka 1972

85. [Inafuta Sheria ya Kanuni za Ufafanuzi wa Sheria na Vifungu vya Ujumla]

___

NYONGEZA

_____

(Kifungu cha 4)

NCHI ZA JUMUIYA YA MADOLA

Antigua and Bermuda
Australia
The Bahamas
Bangladesh
Barbados
Belize
Botswana
Brunei Darusalaam
Canada
Maurishas
Cyprus
Dominica
The Gambia
Ghana
Grenada
Pakistan
Guiyana
India
Jamaika
Kenya
Kiribati
Lesotho
Malawi
Malaysia
Maldives
Malta
Msumbiji
Namibia
Nauru
New Zealand
Nigeria
Papua New Guinea
Visiwa vya Ushelisheli
Sierra Leone
Singapura
Visiwa vya Solomoni
Afrika ya Kusini
Shiri Lanka
St. Kitts and Nevis
St. Lucia
St. Vincent and the Grenadines
Swaziland
Tanzania
Tonga
Trinidad na Tobago
Tuvalu
Uganda
Ufalme wa Uingereza [United Kingdom]
Vanuatu
Samoa ya Magharibi [Western Somoa]
Zambia
Zimbabwe
Rwanda